
# DIVINE BALANCE OF NATURE

ifahamu hekima ya MUNGU katika uumbaji
na upate amani kupitia hekima ya kimungu



BARAKA S BONIVENTURE

# DIVINE BALANCE OF NATURE (Ifahamu hekima ya MUNGU katika uumbaji ili upate Amani kupitia hekim ya mungu)

**© BARAKA S. BONIVENTURE.**

FEBRUARY -2026.

WhatsApp na kawaida: +255 769 924 447

Email:barakaboniventure24@gmail.com

S.L.P 472,

KAHAMA-TANZANIA.

Instagram: barakaboniventure531

Facebook: Baraka Boniventure.

Hauruhusiwi kunakili au kuchukua baaadhi ya kurasa za kitabu hiki bila idhini

**HAKI ZOTE ZIMEHIFADHIWA**

## YALIYOMO


DIBAJI ...................................................................... 6

UTANGULIZI ................................................................ 9

SURA YA KWANZA: MAISHA HALISI DUNIANI ........ 18

Balance of Nature (Urari wa Asili) .................................. 19

Hekima ya Mungu........................................................ 19

Kanuni ya Ufyonzaji na Uhai wa Baada ya Kifo.................. 23

Fumbo la Ghala Lisilokauka Dunia .................................. 24

Ni Rahisi Kukosoa Ukiwa Hauko Mchezoni.................... 27

SURA YA PILI: MWILI WA KRISTO KWENYE DIVINE BALANCE OF NATURE .................................................. 34

Mwili wa Kristo na Siri ya Viungo .................................. 41

Heshima ya Viungo visivyoonekana................................ 47

Sheria ya Majira na Tofauti za Hatua ............................... 48

Mganga Hajigangi........................................................ 50

Usawa wa Kibinadamu na Umuhimu wa Kila Tabaka ..... 57

SURA YA TATU: NGUVU YA USHIRIKIANO (THE POWER OF COLLABORATION) ..................................... 59

Hakuna mchezaji anayeweza kucheza peke yake ............. 59

SURA YA NNE: USICHOKIHITAJI KINAHITAJIKA KWA WENGINE.................................................................... 66

Usichokihitaji Kinahitajika Kwa Wengine ....................... 69

Nguvu ya Pamoja: Jinsi ya Kuthamini Utegemeano Huu. 71

SURA YA TANO: MUNGU HAWEZI KUKUNYIMA VYOTE ........ 73
(The Law of Divine Compensation) ........ 77
Biashara ya Kubadilishana Mapungufu (Trading Our Deficits) ........ 78
SURA YA SITA: WATU WOTE HATUWEZI KUFANIKIWA WOTE KWA SIKU MOJA ........ 81
-Chanzo Cha Ugumu Wa Maisha Ni Ubinafsi ........ 81
Watu Wote Hatuwezi Kufanikiwa Kwa Siku Moja ........ 84
Hakuna Kitu Kinakosesha Raha Kama Kujilinganisha Na Wengine ........ 88
Fumbo la Makao ya Mbegu ardhini ........ 92
Thamani ya Msingi Usioonekana kwa Macho ........ 93
Siri ya Nyakati na Password ya Mafanikio ........ 94
SURA YA SABA: NGA'TA UNACHOWEZA KUTAFUNA ........ 96
Nga'ta Unachoweza Kutafuna ........ 102
SURA YA NANE : MWENYE NGUVU MWITE BINGWA ........ 106
Ng'ata Unachoweza Kutafuna ........ 111
(Usimamizi wa Rasilimali na Subira ya Kimkakati) ........ 114
SURA YA TISA: UNACHOKITUNZA KITAKUTUNZA PIA ........ 116
kanuni ya Kupokea kwa Kutoa (The Law of Reciprocity) ........ 116

Kanuni Ya Kugawana Utajiri ........................................ 118

Unachokitunza Ndicho Kitakachokutunza ...................... 120

Unachokilisha Ndicho Kitakachokulisha ........................ 121

Unachokiheshimu Ndicho Kitakachokutukuza ............... 123

Unachokisamehe Ndicho Kitakachokupa Amani ........... 124

SURA YA KUMI: KUWA NA KIASI KWA KILA JAMBO NI HEKIMA (BALANCE OF EVERYTHING IS WISDOM) ........................................................................... 126

Furahia Kila Hatua Unayopiga Kwenye Maisha (Enjoy Your Life While Living) ............................................... 130

Falsafa ya "Kipimo cha katikati (The Divine Geometry of Balance) ........................................................................ 135

Hatari ya "Kesho Inayouwa Leo" (The Illusion of Tomorrow) ...................................................................... 136

Utajiri wa Roho Dhidi ya Ufukara wa Mali (The Poverty of Having Money) ............................................................ 137

SURA YA KUMI NA MOJA: MWENYE KISU KIKALI NDIYE MLA NYAMA (SURVIVAL FOR THE FITTEST) ........................................................................... 140

Mwenye kisu kikali ndiye mla nyama (Survival of the fittest) ......................................................................... 143

HITIMISHO ..................................................................... 154

**DIBAJI**

Kitabu cha DIVINE BALANCE OF NATURE cha Baraka S. Boniventure kinaeleza hekima ya Mungu katika kuumba ulimwengu, kikilenga kufundisha jinsi ya kupata amani wakati wa shida na umuhimu wa utegemezi wa kibinadamu. Kwa kutumia mifano ya kibaolojia, mwandishi anaonyesha kuwa mapungufu ya kibinadamu yamekusudiwa na Mungu ili kuleta usawa, ushirikiano, na mafanikio katika maisha ya kila mwanadamu.

Hekima hii ya kiungu inatukumbusha kuwa kila dhoruba tunayopitia hubeba kusudi maalum la kutusogeza mbele, sawa na vile dhoruba za asili zinavyosafisha anga na kuleta mvua inayostawisha ardhi. Katika mfumo huu wa maisha, udhaifu wetu sio laana, bali ni mlango wa kutengeneza mahusiano na umoja thabiti na

wenzetu. Tunapokubali mapungufu yetu, tunatoa nafasi kwa wengine kutimiza wajibu wao kwetu, na hivyo kukamilisha mzunguko wa upendo na usawa uliokusudiwa tangu kuumbwa kwa ulimwengu.

Kupitia kurasa za kitabu hiki, msomaji utagundua kuwa maisha hayahitaji ukamilifu wa mtu mmoja, bali yanahitaji ushirikiano wa jamii nzima. Simba hamsemi vibaya swala kwa kuwa mnyonge, na swala hamlaumu simba kwa kuwa mkali; wote wanakiri uwepo wa kila mmoja kama sehemu ya mnyororo wa uzima. Vivyo hivyo, utajiri wa mmoja unakamilishwa na uhitaji wa mwingine, na elimu ya mmoja inajaza ujinga wa mwingine, jambo linalofanya maisha ya mwanadamu kuwa na maana na ladha halisi.

Mwisho kabisa, kitabu hiki kinakupa jicho jipya la kutazama changamoto zako sio kama mwisho wa safari, bali kama sehemu ya "mzani wa maisha" unaokuweka sawa. Unaposoma kazi hii, utatambua kuwa hata katika nyakati za giza nene, mkono wa Mungu usioonekana huwa unarekebisha mambo ili kukurudisha kwenye mstari wako sahihi. Ni matumaini yangu kuwa ujumbe huu utakuwa nanga ya roho yako, ukikupa utulivu wa ndani na hekima ya kukubali, kuheshimu, na kuthamini mchango wa kila mtu unayekutana naye duniani.

# UTANGULIZI

## Ifahamu Hekima ya Mungu katika uumbaji (Understand the wisdom of God in creation)

*Je, umewahi kujiuliza kwa nini vidole vya mkono wako havilingani, lakini vyote ni muhimu ili kuushika mkono wa mwenzako?*

*Kama ulimwengu mzima ungekuwa na majira ya kiangazi pekee, wapi tungepata chemchemi za maji ya kunywa?*

*Ingekuwaje kama kila ndege angetamani kuwa tai; ni nani ambaye angeimba nyimbo za asubuhi kichakani kuamsha ari ya maisha?*

*Je, unafahamu kuwa umaskini wa mmoja ndio unaompa mwingine fursa ya kuwa mkarimu, na utajiri wa mmoja ndio unaompa mwingine fursa ya kupata ajira?*

-----------------------------

**Simulizi na Uhakika wa Kiungu**

Ulishawahi kujiuliza haya maswali mengi labda?

*Hivi ingekuwa watu wote ni matajiri, dunia hii ingekuwa je?*

*Nani angekuwa mfanyakazi wa mwingine?*

*Je, nani angedeki nyumba ya mwenzie?*

*Nani angekuwa mlinzi wa mwenzie?*

*Kama kila mtu angekuwa na kampuni, je, ni nani angekuwa mwajiriwa, na nani angekuwa bosi?*

*Kama kila mtu angekuwa mfanyabiashara, nani angekuwa mnunuzi au mteja, na nani angekuwa mkulima?*

*Au kama watu wote wangekuwa wakulima, je, nani angekuwa mfanyabiashara, na nani angekuwa mnunuzi wa hayo mazao?*

*Je, watu wote wangekuwa mapadre au masista, nani angekuwa mzazi na watu wangeongezekaje duniani?*

*Hekima ya Mungu ni kwamba amefanya kila* kitu kizuri kwa wakati wake. Jua na mwezi huangaza kwa wakati wake; ndivyo ilivyo kwenye maisha yetu, watu wote hatuwezi kufanikiwa kwa kufanya kitu kimoja, bali kila mtu anachokifanya atafanikiwa kwa wakati wake. Hiyo inaitwa the balance of nature (urari wa asili). Mafanikio yako kuna mtu anayasubiri ili na yeye afanikiwe. Haufanikiwi kwa ajili yako peke yako au kwa ajili ya maisha yako tu.

Ndiyo maana mti wa maembe ukizaa sana ni furaha kwa binadamu, lakini pia ni furaha kwa nyani na ndege wa angani. Yesu anaposema tazama ndege wa angani hawapandi wala hawavuni lakini Mungu huwalisha, hiyo ndiyo

maana halisi kwamba katika maisha anaweza kuhangaika mtu mmoja lakini Mungu akamtumia huyo mtu kulisha wengine pia ili wapone na wao kupitia yeye (ndiyo maana halisi ya mkombozi wa familia). Ndiyo maana kuna watu wachache sana hapa duniani ambao kupitia wao Mungu amewatumia kuokoa maisha ya watu wengi sana duniani; mfano Yusufu kule Misri. Hakwenda Misri ili kutajirika na kuota kitambi tu, bali aliende kufanyika lango la wengine, kuokoa maisha yao kutoka kwenye balaa la njaa. Ni muhimu sana kujua sababu ya kwa nini Mungu amekupa mafanikio makubwa kuliko wengine wengi; kumbuka aliyekupa wewe ndiye aliyemnyima mwingine pia.

Ndio maana kuna mtu anaweza kuinuka kiuchumi akawa na kampuni kumi hapa duniani na wakati huo kuna mtu hana hata baiskeli. Hii

inatokea ili huyu ambaye hana baiskeli aende kufanya kazi kwa huyo mwenye kampuni kumi, alipwe mshahara, alishe familia yake na anunue na baiskeli. Huyu wa baiskeli akiwa kwenye level (hatua) ya kufungua makampuni zaidi ya kumi, tayari nyuma yake kutakuwa na watu wengine wengi sana wana hali kama alivyokuwa nayo yeye. That is the meaning of balance of nature. Hakuna siku tutakuwa kwenye level moja. Kila mwaka, kila siku lazima kuwe na ma-gap (nafasi) ili tutegemeane wote.

Hapo ulipo sasa, unaweza usiwe mpango wa Mungu lakini ni mpangilio wa kimungu (divine balance of nature). Kuwepo hapo, hiyo nafasi inahitajika ili kukamilisha kusudi lake la usawa (balance of nature). Unahitajika sana; kwa kujua au kutokujua, uwepo wako una msaada kwa watu unaowajua na usiowajua katika hali yoyote

ile uliyonayo. Sio kwamba ukipata fedha nyingi sana ndipo utaanza kuonekana wa muhimu mbele za Mungu, lahasha! Bali vile ulivyo sasa na kile unachokifanya kikiwa kinampendeza Mungu, basi upo kwenye jukumu zima la kubalance nature.

## Uzuri wa Tofauti Zetu Kama Wimbo wa Ushindi

Katika kwaya kuu ya ulimwengu, uzuri wa wimbo hautokani na waimbaji wote kuimba sauti moja, bali unatokana na muungano wa sauti ya kwanza, ya pili, na ya tatu. Hekima ya Mungu imeweka tofauti kati yetu si kwa ajili ya kutubagua, bali kwa ajili ya kutukamilisha. Kama ulimwengu ungejaa matajiri pekee, utajiri ungepoteza maana yake na kuwa takataka; na kama ungejaa maskini pekee, dunia ingekuwa bonde la vilio. Kila mtu aliyeko chini anasafisha

njia kwa ajili ya aliyeko juu, na aliyeko juu ananyoosha mkono kuwavuta walioko chini. Kitabu hiki kinakukumbusha kuwa, tofauti za kimaisha tulizonazo ni mnyororo wa dhahabu ulioshikamanisha ubinadamu wetu; ukiukata kwa kiburi au kwa malalamiko, unaharibu ramani nzima ya maisha.

## Siri ya Lango na Wajibu wa Kubeba Wengine

Unapoinuliwa na kuwa juu ya wengine, usijidanganye kuwa akili zako au nguvu zako ndizo zilizokufikisha hapo, bali umetengenezwa kuwa "Lango la Baraka." Mungu anapomtafuta mtu wa kumlisha mjane au yatima, hateremki Yeye mwenyewe kutoka mbinguni, bali anaweka fedha hizo kwenye mikono ya mtu mmoja anayemwamini. Yusuf hakupitia mateso ya shimoni na gerezani Misri ili tu aje kuvaa pete ya kifalme, bali alikuwa anaandaliwa kuwa

ghala la uzima kwa ajili ya mataifa yaliyokuwa yanaangamia kwa njaa. Ukubwa wa mafanikio yako hautapimwa kwa idadi ya makampuni unayomiliki, bali kwa idadi ya watu wanaokula, wanaovaa, na wanaosoma kwa sababu wewe upo duniani.

Thamani ya Nafasi Yako ya Sasa Katika Ramani ya Dunia

Mwisho wa siku, lazima utambue kuwa thamani yako haianzi pale unaposhika mamilioni ya fedha, bali inaanza pale unapokubali kutekeleza wajibu wa nafasi uliyopo sasa kwa uaminifu. Hata kama wewe ni mlinzi wa getini, dereva wa bodaboda, au mfanyakazi wa usafi, uwepo wako ni kiungo muhimu sana ambacho kikikosekana, mfumo mzima wa maisha unasimama. Mungu haangalii ukubwa wa jukwaa ulilosimama, bali anaangalia uaminifu wako ukiwa juu ya jukwaa

hilo. Amani ya kweli inapatikana pale unapoacha kushindana na hatua za watu wengine na kuanza kuishi ukijua kuwa, hapo ulipo sasa, wewe ni suluhisho lililotumwa na mbingu kubalance dunia.

# SURA YA KWANZA: MAISHA HALISI DUNIANI

Mnyororo wa maisha ya kibinadamu umefungamanishwa kwa namna ambayo tajiri anamtegemea maskini; tajiri halimi, halali shambani, wala hafanyi kazi zote za mikono. Anahitaji wengine ili maisha yake yaendelee. Vivyo hivyo, maskini anamtegemea tajiri; kupitia ajira, msaada, au huduma zinazotolewa na tajiri, maskini hupata riziki na nafasi ya kuishi.

Hali hii ni sawa na mfano wa mwili wa binadamu: macho hayawezi kufanya kazi ya miguu, wala moyo hauwezi kuchukua nafasi ya mapafu. Kila kiungo kina jukumu lake, lakini vyote vinategemeana ili mwili uishi.

## Balance of Nature (Urari wa Asili)

Kama vile ilivyo katika mazingira ya asili, miti hutengeneza hewa safi kwa ajili ya binadamu na wanyama. Wanyama nao hutegemea mimea kwa ajili ya chakula, na mimea inategemea wanyama kwa ajili ya mbolea na usambazaji wa mbegu. Hata bahari na ardhi zinabadilishana maji kupitia mvua na mito. Huu ndio usawa wa Mungu (the balance of nature)—hakuna kiumbe kinachojitosheleza peke yake.

## Hekima ya Mungu

Mungu aliumba ulimwengu kwa mpangilio wa kutegemeana ili kuondoa kiburi cha kujiona mtu anaweza kufanya kila kitu peke yake. Kila mmoja ana nafasi yake ya kipekee, na hiyo nafasi inahakikisha maisha ya wengine yanaendelea. Tajiri na maskini, bosi na mfanyakazi, wote ni sehemu ya mpangilio wa

Mungu. Japokuwa Mungu hakumuumba mtu akiwa tajiri au maskini, bosi au mfanyakazi—yeye ni Mungu wa wote wenye mwili—lakini hampangii mtu kuwa tajiri au maskini, bali afuataye kanuni alizoweka huyo anakuwa kwenye nafasi fulani. Ndio maana Yesu alisema, "Maskini mnao siku zote." Kumbe maskini hawataisha kwenye maisha yetu na wafanyakazi hawataisha kamwe, lakini ogopa kuwa wa mfano (yaani kuwa mtu asiye na faida katika mfumo).

Ujumbe wa Maisha

Hekima ya Mungu inatufundisha kuwa usidharau nafasi ya mtu mwingine, maana bila yeye huwezi kukamilika. Unamtegemea huyo aidha kwa kujua au kwa kutokujua. Usione aibu kuwa mfanyakazi, maana kazi yako ni sehemu ya mpangilio wa Mungu; bali fanya maamuzi

magumu kupata matokeo adimu mbeleni. Hiyo nafasi uliyopo inakamilisha balance of nature.

Pia, usione fahari kupita kiasi kuwa tajiri, maana bila wengine huwezi kuishi. Elewa hata simba mla swala, naye huliwa pia na bakteria pindi akifa. Hakuna atakayeishi milele, na hakuna aliye juu ya mwenzake; ni swala la nafasi na muda tu (time and chance).

Kwa hiyo, maisha ni mtandao wa kutegemezana na kutegemeana. Ukiwadharau wale uliowaajiri, siku wakiondoka huna kampuni. Ukiwadharau maskini kisa wewe ni tajiri, siku wakiondoka wote duniani hutaishi pia na wewe, maana hakuna atakayelima mazao, hakuna atakayepanda mboga mboga, na hakuna wa kukufanyia kazi yoyote. Maskini naye akimdharau tajiri, siku tajiri akiondoka na yeye mwenyewe maisha yake hayawezi kuwa sawa,

maana wote tunategemeana sana na kutegemezana. No one is an island (Hakuna mtu aliye kisiwa chenyewe). Hii ndiyo the balance of nature.

Nafasi uliyopo inakamilisha balance of nature, lakini pia ukihama hiyo nafasi anakuja mtu mwingine. Na hata ukifa, tayari Mungu alishatengeneza mfumo ambao utaziba nafasi yako. Ndiyo maana swala wanaliwa kila siku huko mwituni na simba, dubu, na wanyama wengine wakali, lakini hutosikia wamepungua hata siku moja. Ndio maana watu wanakula na kufa kila siku lakini hutosikia wamepungua, na kila sensa inayofanyika dunia nzima, idadi ya watu inaongezeka kila mwaka. Dhahabu inachimbwa kila siku lakini hutosikia imeisha. Kwa nini? Kwa sababu ya divine balance of nature (urari wa kimungu wa asili). Nothing will

change the system of God (Hakuna kitakachobadili mfumo wa Mungu), hata kama wanadamu wanabuni mbinu mpya za kuishi, lakini bado hamna kitu cha kupunguza idadi ya watu duniani maana hiyo ni hekima ya Mungu katika uumbaji.

## Kanuni ya Ufyonzaji na Uhai wa Baada ya Kifo

Katika muundo wa ulimwengu, hakuna kitu kinachopotea kabisa, bali kila kitu kinabadilika ili kulisha kitu kingine. Simba anapomfukuza na kumla swala, haifanyiki kwa ukatili, bali ni kwa ajili ya kuhamisha nishati ya uhai ili mnyororo wa pori uendelee kusonga mbele. Simba huyo huyo anapofikia uzee na kufa, mwili wake unakuwa chakula cha viumbe wadogo kama bakteria na mchwa, ambao wanautandaza udongo kwa mbolea inayochipusha majani

mapya ya kulisha swala wengine. Hekima hii inatufundisha kuwa, hata katika viwango vya kijamii, nguvu uliyonayo leo itarudi ardhini kesho; hakuna mtawala anayedumu kwenye kiti chake milele, kwani asili inadai kuwa kila aliyeshiba leo lazima asafishe njia kwa ajili ya atakayekuja kula kesho.

**Fumbo la Ghala Lisilokauka Duniani**

Mwanadamu kwa akili zake fupi mara nyingi huingia hofu akidhani kuwa rasilimali za dunia zitaisha kwa sababu ya matumizi ya kila siku. Hata hivyo, dhahabu, almasi, na mafuta vimeendelea kuchimbwa kwa karne nyingi bila mifereji yake kukauka, kwa sababu mikono ya uumbaji ilifunga mifumo inayojizalisha yenyewe chini ya ardhi. Uhaba tunaouona duniani sio upungufu wa baraka za Mungu, bali ni uhaba wa hekima ya usambazaji na ukarimu kati ya

wanadamu. Mungu anapofungua milango ya ardhi kutoa utajiri, haandiki jina la mtu mmoja kwenye mawe hayo, bali anaiachia dunia ijue kuwa kila kijiko kinachochota kinapaswa kurudisha sehemu ya mchango wake ili kuwasha taa ya wengine.

Kiburi cha mtu aliyeinuka kiuchumi mara nyingi kinatokana na kusahau kuwa yeye ni mpita njia tu ambaye amekuta mfumo ukiwa umesimama na atauacha ukiendelea. Sensa za kila miaka zinapoonyesha kuongezeka kwa watu licha ya magonjwa, vita, na vifo, ni uthibitisho thabiti kuwa hakuna mwanadamu aliye wa kipekee kiasi cha kuzuia jua lisichomoze akiondoka. Nafasi unayoikalia leo kama bosi, kiongozi, au tajiri ni kiti cha kukodisha; ukimaliza muda wako, asili itakusukuma pembeni na kumleta mtu mwingine ambaye hukudhani kama

anaweza. Kutambua ufupi wa uwepo wako na ukubwa wa mfumo wa Mungu kunakutaka uishi kwa unyenyekevu, ukitenda wema kwa walio chini yako, kwani jina lako litasahaulika lakini alama ya usawa uliyoiacha itadumu.

Mwisho wa siku, lazima mwanadamu afahamu kuwa Mungu hachagui nani awe maskini au nani awe tajiri kwa upendeleo, bali ameweka sheria za kiuchumi na kiroho zinazofanya kazi kama mvuto wa ardhi (gravity). Yule anayezitii kanuni za kazi, nidhamu ya kifedha, na uwekezaji anasukumwa kuelekea kwenye nafasi ya utajiri, huku anayezipuuza akiangukia kwenye dimbwi la uhitaji. Hata hivyo, mfumo huu unakamilika pale tu ambapo aliyefanikiwa anatambua kuwa ushindi wake unalindwa na amani ya yule asiyenacho. Mechi ya maisha haichezwi ili

mmoja amfilisi mwenzake, bali inachezwa ili wote kwa pamoja tuweze kumaliza dakika tisini tukiwa salama, kila mmoja akitekeleza wajibu wa kiwango chake kwa utayari na heshima.

## Ni Rahisi Kukosoa Ukiwa Hauko Mchezoni

Nikiwa mtoto, niliwahi kupita sehemu fulani nikakuta mtu amejenga nyumba haijaisha vizuri lakini akahamia. Yaani haina vioo, haina tiles, na ndani hakuna hata sofa sebuleni. Nilianza kuwaambia marafiki zangu, "Huyu jamaa sijui alikuwa ana haraka gani? Yaani nyumba kubwa namna hii haijaisha vizuri yeye tayari kashahamia! Sijui ana matatizo gani. Ilitakiwa ipigwe ukarabati wa hali ya juu kabisa kabla ya kuhamia humo." Tukacheka na wenzangu, wakaongezea, "We ngoja, mimi mjengo wangu utakuwa ni wa mfano kwenye mtaa mzima nitakaokuwa naishi." Maana kipindi hicho

tuliona maisha ni mepesi sana, na kila unachokipanga basi kitaenda hivyo kama ulivyopanga.

Siku zilivyoenda, nimemaliza chuo niko mtaani najitafuta maisha, nikawa nimewaza kununua kiwanja. Naambiwa bei ya kiwanja kidogo, walau 20 kwa 15 unachoweza kujenga nyumba, ni kuanzia milioni tatu na nusu au nne hadi milioni tano. Na mimi nina kama milioni moja tu! Nikaenda mbali zaidi nikauliza gharama ya tofali, nikaambiwa tofali moja kwa sasa ni 1,300. Kuuliza tripu moja ya mawe naambiwa elfu tisini. Nikawa nawaza kichwani, ili nyumba iishe yote itanichukua fedha kiasi gani kwa namna hii? Maana kila kitu kipo juu sana, hapo bado bati sijauliza, nondo, tiles na kadhalika.

Ndipo Roho wa hekima akanambia, "Unakumbuka kipindi kile mnaambizana wewe

na rafiki zako kwamba yule mtu aliyejenga nyumba hakumalizia vitu vya ndani akawa amehamia mkamwona kama mjinga? Sasa, huu ndio uhalisia wa maisha sasa." Akasema, "Ni rahisi sana kukosoa ukiwa hauko mchezoni. Utaona kuna makosa, utaona kitu chepesi sana maana huwezi kujua uzito wa kiatu ambacho hujakivaa." Kuna watu wengi sana huwa wanawalaumu viongozi lakini ukiwachunguza maisha yao, hawajawahi hata kuwa ma-monitor wa darasani au hata mabalozi wa nyumba kumi, lakini utakuta wanamnyooshea kidole Rais wa nchi anayeongoza mamilioni ya watu!

Kama ambavyo kwenye mchezo wa mpira wa miguu mashabiki hulalamika sana ikitokea mchezaji amekosa goli, lakini ukimchukua shabiki mmoja ukamwambia ingia na wewe uwanjani ukafunge goli, unaweza kumshangaa

mpira unaisha dakika tisini hata kugusa mpira hajagusa! Kama kiatu hujakivaa huwezi kujua uzito wake, hivyo ni hekima kunyamaza kama haupo kwenye ulingo wa mapambano. Until you are there, just keep quiet (Hadi utakapofika hapo, baki kimya). Kuanzia hapo nilianza kunyamaza kimya nilipoona mtu anashindwa kufanikiwa, au haendelei mbele, au anafanya vitu chini ya kiwango, maana sijui kiatu alichokivaa.

## Maktaba ya Hekima Kuhusu Uhalisia wa Ulingo wa Maisha

Katika jumba la maisha, kuna utofauti mkubwa sana kati ya mtu anayetazama mchezo kutoka jukwaani na yule anayepambana katikati ya uwanja. Shabiki ana faida ya kuona makosa ya kila mtu kwa sababu yeye hajakumbana na upepo, kigingi, au shinikizo la muda

linalomkabili mchezaji. Hekima ya kitabu hiki inatufundisha kuwa, maneno ya mkosoaji mara nyingi huwa hayana uzito kwa sababu hayajapita kwenye tanuru la uhalisia. Ni rahisi kupanga ramani ya vita ukiwa umekaa sebuleni kwako kwa amani, lakini ukiingizwa mstari wa mbele ambako risasi zinalia, hata mbinu zako zilizoonekana bora zinasahaulika. Mtu mwenye hekima hujifunza kutoshabikia kapu la mtu mwingine lililo tupu, hadi pale atakapobeba la kwake na kuona jinsi kamba inavyokata bega lake.

## Sheria ya kunyamaza na Heshima kwa Mapambano ya Wengine

Unyamavu mbele ya juhudi za mtu mwingine siyo uoga, bali ni kiwango cha juu cha ukomavu wa kiakili na kiroho. Kila mwanadamu anapita kwenye vita vyake vya siri ambavyo jamii

haivijui; mmoja anapambana kupata tofali moja, mwingine anapambana kulipa ada, na mwingine anapambana kuzuia kampuni isife.

Unapomwona mtu amesimika boma lake bila paa akahamia, usimhukumu kwa macho ya nje; huyo ni shujaa aliyeshinda vita vya kupanga na sasa anapambana kulinda heshima yake. Kitabu hiki kinakusihi uweke akiba ya maneno yako unapoona matokeo ya chini ya kiwango kutoka kwa mwenzako. Badala ya kunyoosha kidole cha lawama, jifunze kuheshimu jasho la mtu anayejaribu kufanya kitu, kwani mchango mdogo uliokamilika ni bora mara mia kuliko ndoto kubwa ambayo haijawahi kuanza.

## Kipimo cha Uongozi na Gharama ya Maamuzi

Mwisho wa siku, uzito wa taji haujulikani na yule anayelitazama likiwa kichwani mwa

mfalme, bali unajulikana na yule anayebeba maumivu ya shingo yake. Kuongoza maisha yako mwenyewe, familia yako, au taifa zima kunahitaji maamuzi magumu ambayo mara nyingi hayatafurahiwa na mashabiki wa nje. Ni rahisi kumlaumu Rais au kiongozi yeyote ukiwa umekaa kijiweni, kwa sababu huna mzigo wa kubeba lawama za mamilioni ya watu kesho asubuhi. Kabla hujakaribisha roho ya ukosoaji juu ya mtu aliyeko juu yako, jiulize kama umeweza kusimamia vema kile kidogo ulichokabidhiwa. Ulingo wa maisha hauhitaji waamuzi wengi wa maneno; unahitaji wapiganaji wenye unyenyekevu wanaojua kuwa, hata kama hatua ni ndogo kiasi gani, bora ni yule anayetembea kuliko yule aliyekaa chini akicheka wanaojikita.

## SURA YA PILI: MWILI WA KRISTO KWENYE DIVINE BALANCE OF NATURE

Kwenye mwili wa binadamu kuna viungo vingi sana — vingine vinaonekana, vingine havionekani; vingine vina heshima, vingine havina heshima.

> “Kwa maana mwili si kiungo kimoja, bali ni vingi. Mguu ukisema, ‘Kwa kuwa mimi si mkono, mimi si wa mwili,’ je, si wa mwili kwa sababu hiyo? Na sikio likisema, ‘Kwa kuwa mimi si jicho, mimi si la mwili,’ je, si la mwili kwa sababu hiyo? Kama mwili wote ukiwa jicho, ku wapi kusikia? Kama wote ni sikio, ku wapi kunusa?”

Mungu ameviweka viungo kila kimoja katika mwili kama alivyotaka. Kama vyote vingekuwa kiungo kimoja, mwili ungekuwa wapi?

Sasa viungo ni vingi, ila mwili ni mmoja.

Jicho haliwezi kuuambia mkono, “Sina haja na wewe,” wala kichwa hakiwezi kuiambia miguu, “Sina haja na ninyi.”

Bali zaidi sana, vile viungo vya mwili vinavyodhaniwa kuwa vinyonge zaidi, ndivyo vinavyohitajika zaidi.

Mungu ameunganisha mwili kwa hekima, akakipa heshima zaidi kile kiungo kilichopungukiwa, ili kusiwe na faraka katika mwili, bali viungo vitunzane kila kimoja na mwenziwe.

Kiungo kimoja kikiumia, viungo vyote huumia nacho; na kiungo kimoja kikitukuzwa, viungo vyote hufurahi pamoja nacho.

Ndiyo maana ikitokea msiba wa ndugu yetu au mtu yeyote duniani, watu wote huomboleza na kusema “pengo lake haliwezi kuzibika.”

Kwa sababu katika balance of nature, kila mtu ana nafasi yake, na kila kiumbe kina umuhimu wake katika dunia hii.

Basi ninyi mmekuwa mwili wa Kristo, na viungo kila kimoja peke yake.

Kama viungo katika mwili wa Mungu, tunategemeana sana — hakuna aliye bora zaidi ya mwenzake.

Leo, watu wenye makampuni makubwa kama Elon Musk, Bill Gates, na Steve Jobs wanajulikana sana, na huonekana kuwa na mchango mkubwa katika maisha ya watu.

Lakini kuna mama mmoja mtembeza mihogo au mchicha kila asubuhi, anayewaokoa watu wengi na njaa — ingawa hafahamiki.

Kuna dada mmoja mgahawanayepika chakula kwa bidii ili waendesha bodaboda wasife njaa wakati wa kutafuta riziki.

Siku moja Mungu akisema awaondoe watu hao wa chini, itakuwa sawa na kukata kiungo kisichoonekana kwenye mwili wako.

Unajua sehemu za siri za mwili wako zilivyo na umuhimu mkubwa kuliko hata mikono, miguu, maskio au pua — lakini havionekani hadharani.

Kwa sababu havionekani, mtu anaweza kudhani havina heshima, lakini Mungu, Mfalme wa Balance of Nature, anajua umuhimu wake.

Ili maisha yabalance, lazima kuwe na boda boda — kumwahisha msafiri; lazima kuwe na mama ntilie — kumpa chakula mwenye njaa; lazima kuwe na muuza mitumba — kumsaidia mwenye

kipato cha chini kupata nguo za kumstiri; lazima kuwe na mwenye nyumba ya kupangisha — kumpa makazi asiyeweza kujenga kwa wakati huo.

Kosa kubwa tunalofanya wanadamu ni kumdharau mtu aliye chini, tukimwona kama mkosefu au asiye na akili timamu.

Tunapaswa kukumbuka kwamba jua na mwezi haviwezi kuangaza kwa wakati mmoja.

Watu wote hawawezi kuwa na hali moja ya maisha — hata Mungu mwenyewe hawezi kuruhusu hilo.

Japokuwa mwanzo alituumba tuwe na hali sawa, baada ya dhambi ya ujana kule Edeni mambo yalibadilika.

Hatutakuwa sawa hata siku moja, kwa sababu Mungu anabalance nature kwa hekima yake.

Kama chuoni hatumalizi wanafunzi wote kwa mwaka mmoja, ndivyo ilivyo kwenye

Maisha:

- Mwingine anamaliza chuo, mwingine anaingia mwaka wa kwanza.

- Mwingine ana miaka mitano kazini, mwingine anaanza kutafuta ajira.  Mwingine anastaafu.

- Mwingine anamaliza kujenga nyumba, mwingine anaanza kampuni.  Huyu mwingine ana tafta chumba Cha kupanga

- Mwingine anawaza atatoa wapi kodi ya nyumba.

Mwingine anamaliza nyumba ya tatu ya kupangisha

Lakini habari njema ni kwamba kila mtu yupo kwenye safari yake ya mafanikio, na kila mtu

atafanikiwa kwa wakati wake — ni suala la muda tu.

Maisha ni kutegemeana.  Kila mtu amepewa limitation na Mungu ya kufanya mambo fulani. Unaweza kujitutumua kadri uwezavyo, lakini hutafanya kila kitu.

Tajiri anamtegemea maskini, na maskini anamtegemea tajiri ili kuishi.

Tajiri halimi — maskini ndiye anayelima na kulipwa mshahara.  Duniani kote tulipitia hali ya ya kuongezeka kwa Bei ya mafuta , sababu zilizotajwa ni kwamba ni vita ya Ilan na Israel akashirikiana na marekani ,nikawa nawaza kichwani yani wapigane wengine halafu madhara yake yatupate Dunia nzima , wakati haya ni mabara matatu tofauti kabisaa. Ndipo nikagundua kumbe wanadamu wote tunategemeana haijalishi kwenye mazingira

Gani na eneo lipi ulilopo, tunategemeana sana ni viungo katika mwili wa MUNGU,

**Mwili wa Kristo na Siri ya Viungo**

Kwenye mwili wa binadamu kuna viungo vingi sana; vingine vinaonekana, vingine havionekani, vingine vina heshima na vingine havina heshima. Kama Maandiko yanavyosema:

“Kwa maana mwili si kiungo kimoja, bali ni vingi. Mguu ukisema, Kwa kuwa mimi si mkono, mimi si wa mwili; je! Si wa mwili kwa sababu hiyo? Na sikio likisema, Kwa kuwa mimi si jicho, mimi si la mwili; je! Si la mwili kwa sababu hiyo? Kama mwili wote ukiwa jicho, ku wapi kusikia? Kama wote ni sikio ku wapi kunusa? Bali Mungu amevitia viungo kila kimoja katika mwili kama alivyotaka. Lakini kama vyote vingekuwa kiungo kimoja, mwili ungekuwa wapi? Lakini sasa viungo ni vingi, ila

mwili ni mmoja. Na jicho haliwezi kuuambia mkono, Sina haja na wewe; wala tena kichwa hakiwezi kuiambia miguu, Sina haja na ninyi. Bali zaidi sana vile viungo vya mwili vidhaniwavyo kuwa vinyonge zaidi vyahitajiwa zaidi. Na vile viungo vya mwili vidhaniwavyo kuwa havina heshima, viungo vile twavipa heshima zaidi; na viungo vyetu visivyo na uzuri vina uzuri zaidi sana. Kwa maana viungo vyetu vilivyo na uzuri havina uhitaji; bali Mungu ameuungamanisha mwili, na kukipa hesh ima zaidi kile kiungo kilichopungukiwa; ili kusiwe na faraka katika mwili, bali viungo vitunzane kila kiungo na mwenziwe. Na kiungo kimoja kikiumia, viungo vyote huumia nacho, na kiungo kimoja kikitukuzwa, viungo vyote hufurahi pamoja nacho." — 1 Wakorintho 12:14-26

Ndiyo maana ikitokea msiba wa ndugu yetu au mtu yeyote duniani, watu wote lazima tuomboleze na kusema pengo lake haliwezi kuzibika. Hii ni kwa sababu kwenye balance of nature (urari wa asili), kila mtu ana nafasi yake kwenye maisha na kila kiumbe kina umuhimu wake katika hii dunia.

Basi ninyi mmekuwa mwili wa Kristo, na viungo kila kimoja peke yake. Kama viungo katika mwili wa Mungu, tunategemeana sana; hakuna aliye bora zaidi ya mwenzake. Nafahamu fika kwa sasa watu wenye makampuni makubwa kama kina Elon Musk, Bill Gates, na kina Steve Jobs ndio wanaojulikana sana na pengine huonekana wa maana na wenye mchango mkubwa sana kwenye maisha ya watu. Lakini kuna mama mmoja mtembeza mihogo au mchicha kila siku na chai

asubuhi huokoa watu wengi sana na njaa asubuhi lakini hafahamiki. Kuna dada mmoja yuko busy (anashughulika) kupika chakula mgahawani kusaidia waendesha bodaboda ili wasife na njaa wakati wa utafutaji.

Siku moja Mungu akisema awaondoe (awaondoe) hao watu walio chini, ndiyo itakuwa sawa na kuamua kukata kiungo kisichoonekana kwenye mwili wako. Nafahamu fika unajua sehemu za siri za mwili wako zilivyo na umuhimu zaidi kuliko hata mikono na miguu, kuliko hata masikio na pua, lakini havionekani hadharani. Ila kwa kuwa havionekani, mtu anaweza kusema havina umuhimu au heshima zaidi, lakini Mungu—the King of balance of nature (Mfalme wa urari wa asili)—anajua umuhimu wake.

Ili maisha ya-balance (yawe na usawa), lazima pawe na bodaboda ili kumwahisha mtu anayesafiri kwenda sehemu moja au nyingine. Lazima kuwe na mama ntilie, lazima awepo wa bajaj, na lazima awepo muuza mitumba ili kumsaidia yule mwenye kipato cha chini kupata nguo za kumstiri mwili wake asitembee uchi. Lazima awepo mtu mwenye nyumba ya kupangisha ili watu ambao hawana fedha za kujenga kwa wakati huo wapate hifadhi na sehemu ya makazi. Kosa kubwa tunalolifanya wanadamu wote ni kumdharau mtu ambaye yuko chini na kumwona kama mkosefu au hana akili timamu. Ila tunasahau ya kuwa jua na mwezi haviwezi kuangaza kwa wakati mmoja. Watu wote hawezi kuwa na hali moja ya maisha, hata Mungu mwenyewe hawezi kuruhusu hilo.

Japokuwa mwanzo alituumba wanadamu wote tuwe na hali sawa ya maisha, lakini baada ya kutenda dhambi ya asili kule Edeni, mambo yalibadilika; hatutakuwa sawa hata siku moja, Mungu itamuwia ugumu kubalance nature (kama tukiwa sawa). Hii ni kama ambavyo chuoni hatumalizi wanafunzi wote kwa siku moja au kwa mwaka mmoja; bali mwingine akiwa anamaliza chuo, mwingine ananza mwaka wa kwanza. Mwingine tena ana miaka mitano yuko kazini, na mwingine ndio anaingia mtaani kuhangaikia ajira. Maisha ndivyo yalivyo, hatutakuwa sawa hata siku moja. Jinsi tunavyoachana kidato, ndivyo tunavyoachana kwenye maisha pia. Mmoja akiwa anamaliza kujenga nyumba nzuri ya kuishi, mwingine ameshaanza kampuni au kiwanda; mwingine akiwa anamaliza nyumba ya kupangisha, kuna mwingine anawaza atatoa wapi kodi ya nyumba.

Lakini habari njema ni kwamba kila mtu yupo kwenye safari ya mafanikio na kila mtu atafanikiwa kwa wakati wake. Ni swala la muda tu.

Maisha tunategemeana. Kila mtu amepewa limitation (ushahidi wa kikomo) na Mungu ya kufanya vitu; yaani unaweza kujitutumua kadiri uwezavyo lakini hutafanya kila kitu. Tajiri anamtegemea maskini na maskini anamtegemea tajiri ili kuishi. Tajiri halimi, maskini ndiye anayelima na kulipwa mshahara

**Heshima ya Viungo visivyoonekana**

Katika muundo wa kimungu, ustawi wa mfumo mzima hautegemei viungo vinavyopigiwa makofi hadharani, bali unalindwa na viungo vinavyofanya kazi kwa siri chini ya nguo. Dunia inaweza kuwashangilia wavumbuzi wa teknolojia na mamilionea walio juu ya

majukwaa, lakini misingi ya uhai wa kila siku inashikiliwa na mikono yenye malengelenge ya wakulima, jasho la mama ntilie, na uaminifu wa madereva wa bodaboda. Hekima ya uanaume na utu inatutaka kutodharau unyenyekevu wa kazi ya mtu mwingine; kwani kama vile moyo usivyoonekana kwa nje lakini ukisimama kwa sekunde moja mwili mzima unakufa, ndivyo na mchango wa watu "wadogo" kijamii ulivyo nguzo kuu ya kuendesha ulimwengu wetu.

**Sheria ya Majira na Tofauti za Hatua**

Maisha hayakuumbwa kuwa mbio za uwanjani ambako kila mtu anaanza na kumaliza kwenye mstari mmoja kwa wakati mmoja, bali ni mfumo wa zamu na majira ya kimungu. Unapomwona mwenzako anapambana kulipa kodi ya chumba kimoja wakati wewe unamaliza boma la ghorofa, usimnyooshee kidole cha dharau, kwani

kila mtu yuko kwenye darasa lake la maisha na anasoma ukurasa wake. Tofauti za nyakati zetu za kufanikiwa hazimaanishi kuwa mmoja amefeli na mwingine ameshinda, bali ni mpangilio mzuri unaohakikisha kuwa dunia haikosi walimu kwa sababu kila mtu amekuwa mwanafunzi kwa wakati wake. Kujua siri hii kunaleta amani ya moyo; kunakuondolea kiburi unapokuwa juu na kunakupa matumaini unapokuwa chini, ukijua kuwa zamu yako inakuja.

## Mnyororo wa Utegemezi na Kikomo cha Kibinadamu

Mwisho wa siku, Mungu ameweka kikomo (limitation) ndani ya kila mwanadamu ili kuzuia roho ya ubinafsi na kujidai. Hata uwe na utajiri wa kununua mji mzima, huwezi kujilimua chakula chako mwenyewe, huwezi kujijengea

nyumba peke yako, na huwezi kujizika siku ukifa. Utajiri wa tajiri unakamilishwa na nguvu kazi ya maskini, na mahitaji ya maskini yanatimizwa na mtaji wa tajiri. Huu ndio mzani kamili wa asili unaotufundisha kuwa sote ni viungo vya mwili mmoja wa Kristo. Kulinda heshima ya mwenzako, bila kujali kiwango chake cha sasa cha kiuchumi, ni kutambua kuwa ustawi wako umejificha ndani ya uwepo wake.

**Mganga Hajigangi**

MUNGU alituumba wanadamu kuishi kwa kutegemeana siku Moja eliya alikua na njaa jangwani MUNGU akamwambia aende serpta kwa mama mmoja

mjane, alipofika kwa mama huyo mjane akamwambia na njaa nitengenezee chakula Nile yule mama akasema Mimi na mkate mmoja tu nakula na mwanangu Leo nife kabisaa lakini

eliya akamwambia nitengenezee chakula Nile, baadae yule mwanamke akatii baada ya kutenda jambo lile chakula kiliongezeka na wakala siku nyingi sana,

Swali la kujiuliza kwa nini eliya aliambiwa aende kwa mjane, ikiwa MUNGU alikua ana uwezo wa kumlisha jangwani na hakufanya jambo Hilo mara Moja maana alikua ana mlisha eliya kwa kutumia kunguru,

Kitu kikubwa Sana tunachotakiwa kujua kuwa MUNGU hakumuumba Mtu Aishi kwa kujitenga ,alituumba Tuishi kwa kutegemeana, ndiyo maana MGANGA HAJIGANGI, daktari hawezi kujitibu ,mkunga hawezi kujizalisha , mwalimu hawezi kujifundisha tuliumbwa kutegemeana ndiyo maana wachungaji na watumishi wa MUNGU waliambiwa watakula madhabahuni, kwa sababu wao wako busy

kutafta uso wa MUNGU na kuwatumikia watu wake hivyo mahitaji Yao pia Mungu aliamuru watu wengine wayatimize ndio maana MUNGU akasema makuhani watakula madhabahuni, this is the meaning of balance of nature, ndio maana ni muhimu Sana ukajua watu wengine walio juu yako au chini Yako wanaokutegemea ili uwasaidie maana kwenye balance of nature Tunaishi kwa kutegemeana,hakuna MTU anaweza kuishi peke yake bila kutegemezana.

Kwa uwezo wa eliya alikua anaweza kumuomba MUNGU akashusha mkate Toka mbinguni lakini aliambiwa naenda kwa mjane ukale huko hiyo ilikua ishara ya kutegemezana na kutegemeana. Mjane akatoa chakula eliya akazidisha chakula mwisho wa siku wakala wote wakashiba, MGANGA HAJIGANGI, daktari hawezi kujitibu mkunga hawezi kujizalisha, hii

ni hekima ya MUNGU kwenye balance of nature.

## Mganga Hajigangi

Mungu alituumba wanadamu kuishi kwa kutegemeana. Siku moja Eliya alikuwa na njaa jangwani, Mungu akamwambia aende Sarepta kwa mama mmoja mjane. Alipofika kwa mama huyo mjane, akamwambia, "Nina njaa, nitengenezee chakula nile." Yule mama akasema, "Mimi nina mkate mmoja tu, nakula na mwanangu leo nife kabisa." Lakini Eliya akamwambia, "Nitengenezee chakula nile." Baadaye yule mwanamke akatii. Baada ya kutenda jambo lile, chakula kiliongezeka na wakala siku nyingi sana.

Swali la kujiuliza: kwa nini Eliya aliambiwa aende kwa mjane, ikiwa Mungu alikuwa na uwezo wa kumlisha jangwani na hakufanya

jambo hilo mara moja, maana alikuwa anamlisha Eliya kwa kutumia kunguru? Kitu kikubwa sana tunachotakiwa kujua ni kuwa Mungu hakumuumba mtu aishi kwa kujitenga; alituumba tuishi kwa kutegemeana. Ndiyo maana MGANGA HAJIGANGI, daktari hawezi kujitibu, mkunga hawezi kujizalisha, na mwalimu hawezi kujifundisha. Tuliumbwa kutegemeana, ndiyo maana wachungaji na watumishi wa Mungu waliambiwa watakula madhabahuni. Hii ni kwa sababu wao wako busy (wanajishughulisha) kutafuta uso wa Mungu na kuwatumikia watu wake, hivyo mahitaji yao pia Mungu aliamuru watu wengine wayatimize; ndio maana Mungu akasema makuhani watakula madhabahuni. This is the meaning of balance of nature (Hii ndiyo maana ya urari wa asili). Ndio maana ni muhimu sana ukajua watu wengine walio juu yako au chini yako wanaokutegemea

ili uwasaidie, maana kwenye balance of nature tunaishi kwa kutegemeana; hakuna mtu anaweza kuishi peke yake bila kutegemezana.

Kwa uwezo wa Eliya, alikuwa anaweza kumuomba Mungu akashusha mkate kutoka mbinguni, lakini aliambiwa, "Nenda kwa mjane ukale huko." Hiyo ilikuwa ishara ya kutegemezana na kutegemeana. Mjane akatoa chakula, Eliya akazidisha chakula, mwisho wa siku wakala wote wakashiba. MGANGA HAJIGANGI, daktari hawezi kujitibu, mkunga hawezi kujizalisha; hii ni hekima ya Mungu kwenye balance of nature.

## Sauti ya Hekima Kuhusu Fumbo la Kiroho la Mifereji na Visima

Katika ulimwengu wa roho, hakuna mwanadamu aliyeumbwa kuwa bahari inayopokea maji bila kutoa; badala yake, tuliumbwa kuwa mifereji

inayopitisha baraka. Hekima ya kimungu ilimweka Eliya na yule mjane wa Sarepta katika mzani mmoja ili kudhihirisha kuwa, mara nyingi ufunguo wa muujiza wako hauko mikononi mwako, bali uko mikononi mwa mtu mwingine anayekuhitaji. Eliya alikuwa na upako lakini alikuwa na njaa; mjane alikuwa na unga lakini alikuwa na hofu ya kifo. Kiroho, Mungu anaunganisha uhitaji wa mmoja na ziada ya mwingine ili kutengeneza mzunguko wa uzima. Unapojaribu kuwa kisima kinachojitegemea, unakiuka sheria ya kiroho ya ukarimu na unajihukumu kukauka, kwani baraka ya kweli haitiririki kwa anayelundika, bali kwa anayekuwa kiunganishi cha wengine.

## Usawa wa Kibinadamu na Umuhimu wa Kila Tabaka

Katika maisha yetu ya kawaida ya kijamii, kanuni ya "Mganga Hajigangi" inatukumbusha kuwa vyeo, mamlaka, na utajiri wetu ni vitu visivyo na nguvu bila uwepo wa watu wengine. Tajiri mkubwa anahitaji mkulima wa kijijini ili apate chakula mezani kwake, na mfalme anahitaji walinzi ili alale kwa amani usiku. Hii inatufundisha unyenyekevu mkubwa: hakuna mwanadamu aliye mdogo sana kiasi cha kutomhitaji, na hakuna aliye mkubwa sana kiasi cha kutojulikana udhaifu wake. Maisha ni mtandao uliosukwa kwa ufundi wa hali ya juu; ukikata uzi mmoja wa wale walio chini yako, unaharibu taswira nzima ya usalama wako mwenyewe. Kuthamini wanaokutegemea na wale unaowategemea ndiyo siri pekee ya kudumisha amani na ustawi wa kijamii duniani.

## Ukombozi wa Pamoja na Hatma ya Kibinadamu

Mwisho wa siku, hatma ya mwanadamu haisomeki kwa jinsi anavyoishi peke yake, bali kwa jinsi anavyogusa na kubadilisha maisha ya wengine. Kama Eliya angejifungia jangwani akiomba mikate ishuke, angebaki peke yake na muujiza wake, lakini kwa kwenda kwa mjane, alikomboa familia nzima kutoka kwenye janga la njaa. Hekima kuu ya kitabu hiki inakutaka utambue kuwa, kufanikiwa kwako kuna maana pale tu kunapomsaidia mtu mwingine kusimama. Tunaposaidiana kubeba mizigo, safari inakuwa fupi na ushindi unakuwa wa pamoja. Kubali kuwa unahitaji msaada, na uwe tayari kuwa msaada kwa wengine; hiyo ndiyo kanuni kuu inayolinda ulimwengu isisambaratike, na ndio mtindo wa maisha unaoacha alama isiyofutika vizazi na vizazi.

## SURA YA TATU: NGUVU YA USHIRIKIANO (THE POWER OF COLLABORATION)

Maisha ni sawa na mchezo wa mpira wa miguu ambao hauishi kwa dakika tisini, yaani maisha ni mechi isiyo Isha Hadi siku unakufa, ukitazama vizuri mchezo wa mpira wa miguu unaweza kujifunza mambo mazuri Sana, maana ndivyo maisha yetu ya kila siku yalivyo.

### Hakuna mchezaji anayeweza kucheza peke yake

Kama ambavyo hakuna mchezaji anayeweza kutoka Gori moja na Mpira Hadi Gori jingine na Kufunga ndivyo ambavyo hakuna MTU anaweza kufanya kila kitu peke yake na kufanikiwa kwenye maisha, kila goli linaloshangiliwa na mashabiki nyuma yake Huwa Kuna assist , yani msaidizi wa Kufunga

like Gori , NDIO maana Kuna team ambazo hucheza kwa pasi yani mpira unatoka kwa MTU huyu na kwenda kwa mwingine Huwa zinasifika kwa kupata ushindi wa mara kwa mara maana Wana tii kanuni ya collaboration, no one can obtain success alone, hata kama uwe na kiwango cha kina Christian Leonardo au kina mess lakini bado huwezi kucheza peke Yako uwanjani na hata ukisema uingie uwanjani ukae na Mpira wewe peke Yako bado hutaweza kuifanya team ishinde badala yake wewe mwenyewe hutafunga na pengine kujisababishia majera na team pia haitafunga.

Maisha ni game of collaboration, huyu anapiga chenga ana mpasia huyu na mwingine anafunga , kitendo Cha team Kufunga wote mmefunga maana team yenu inakua imeshinda pia.

Maisha ni sawa na mchezo wa mpira wa miguu ambao hauishi kwa dakika tisini; yaani maisha ni mechi isiyoisha hadi siku unakufa. Ukitazama vizuri mchezo wa mpira wa miguu, unaweza kujifunza mambo mazuri sana maana ndivyo maisha yetu ya kila siku yalivyo. Katika uwanja wa maisha, hakna mchezaji anayeweza kucheza peke yake na akafanikiwa kuisogeza timu mbele. Kama ambavyo hakuna mchezaji anayeweza kutoka goli moja na mpira hadi goli jingine na kufunga, ndivyo ambavyo hakuna mtu anayeweza kufanya kila kitu peke yake na kufanikiwa kwenye maisha. Kila goli linaloshangiliwa na mashabiki nyuma yake huwa kuna pasi ya usaidizi, yaani assist, ambayo ni mchango wa mtu mwingine aliyewezesha lile goli kufungwa. Ndio maana kuna timu ambazo hucheza kwa pasi, ambapo mpira unatoka kwa mtu huyu na kwenda kwa mwingine; timu hizi

huwa zinasifika kwa kupata ushindi wa mara kwa mara maana zinatii kanuni ya ushirikiano (collaboration). Hakika, hakuna mtu anayeweza kupata mafanikio peke yake (no one can obtain success alone). Hata kama uwe na kiwango kikubwa cha kina Cristiano Ronaldo au kina Lionel Messi, bado huwezi kucheza peke yako uwanjani. Hata ukisema uingie uwanjani ukae na mpira wewe peke yako, bado hutaweza kuifanya timu ishinde; badala yake wewe mwenyewe hutafunga, utajisababishia majeraha, na timu pia haitafunga. Maisha ni mchezo wa ushirikiano ambapo huyu anapiga chenga, anampasia huyu, na mwingine anafunga. Kitendo cha timu kufunga maana yake wote mmefunga, kwa sababu timu yenu inakuwa imeshinda pia.

Ili wasomaji waelewe kwa kina nguvu hii ya ushirikiano, ni vyema kutazama jinsi kanuni hii

inavyofanya kazi kwa watu waliofanikiwa na kwenye mifumo mikubwa ya kiuchumi kama vile ununuzi wa hisa benki. Watu wote waliopo kileleni mwa mafanikio duniani kote wamegundua siri moja kubwa: talanta ya mtu mmoja inaweza kushinda mechi, lakini ushirikiano na akili ya timu nzima ndio inayoshinda vikombe. Falsafa hii inajidhihirisha vyema kupitia mfumo wa hisa kwenye mabenki na makampuni makubwa. Hisa moja ya benki inaweza kuwa na thamani ndogo sana inayoweza kununuliwa hata na mtu wa kipato cha chini. Hata hivyo, mamia au maelfu ya watu binafsi wanapounganisha mitaji yao midogo kupitia ununuzi wa hisa hizo, wanatengeneza mtaji mkubwa wa mabilioni ya fedha. Mtaji huu wa pamoja ndio unaoiwezesha benki kujenga majengo, kutoa mikopo mikubwa, na kuzalisha faida kubwa ambayo mwisho wa siku

inagawanywa tena kwa kila mwanahisa kulingana na mchango wake. Huu ni uthibitisho tosha kwamba umoja sio tu dhana ya kijamii, bali ni nguvu halisi ya kiuchumi inayoweza kugeuza rasilimali ndogo kuwa himaya kubwa ya mafanikio.

Ukiangalia makampuni makubwa yanayoongozwa na watu waliofanikiwa zaidi duniani, kama vile Apple au Microsoft, utagundua kuwa waanzilishi wake hawakuwa wataalamu wa kila kitu. Walichofanya ni kukusanya timu ya watu wenye vipaji tofauti lakini wanaochangia lengo moja. Tajiri au kiongozi anaweza kuwa na maono na mtaji, lakini anahitaji mhandisi wa kutengeneza bidhaa, mhasibu wa kulinda fedha, na mtaalamu wa masoko wa kuifikisha bidhaa kwa wateja. Katika mfumo huu wa maisha, kila mmoja

anakuwa ametoa assist kwa mwenzake. Kitendo cha kampuni kupata faida kinakuwa ni ushindi wa pamoja, kama ilivyo kwa timu ya mpira inayoshinda kikombe. Binadamu anayejaribu kufanya kila kitu peke yake anajidanganya na anajisababishia msongo wa mawazo na kufeli, sawasawa na mchezaji mchoyo anayevunjiwa miguu uwanjani kwa kung'ang'ania mpira. Wasomaji wanapaswa kuelewa kuwa ili kupiga hatua kubwa maishani, ni lazima wajifunze kuheshimu, kuthamini, na kuwekeza kwenye nguvu ya umoja na ushirikiano, kwani hiyo ndiyo kanuni kuu inayotawala mafanikio endelevu duniani.

## SURA YA NNE: USICHOKIHITAJI KINAHITAJIKA KWA WENGINE

Kuna siku nilikuwa kijijini navuna mahindi yangu. Wakati wa mavuno, wakulima wenzangu wanajua mvua haitakiwi kabisa kwa sababu inaharibu mazao. Kuna siku nilikuwa nimevuna, nikayaanika juani yakauke, mara ghafla ikaanza kunyesha mvua. Nikatafuta turubai kufunika hayo mazao, moyoni nikiomba mvua ikatike. Wakati huo huo, kuna wakulima wa mpunga ambao ulikuwa umekaa siku nyingi bila kupata maji, walikuwa wakiomba: "Mvua nyesha, mvua nyesha!"

Kuna mtu anachukia mvua kwa sababu ya kazi anayoifanya, lakini kuna watu wengine wanakesha kuombea mvua inyeshe kwa wakati

huo huo. Sasa, nani apewe hitaji lake na nani aachwe? Kuna muda bei ya sukari ilipanda sana na watu wakaanza kulalamika kuwa bei ya sukari iko juu, serikali ipunguze kwa sababu watu wanashindwa kuimudu. Lakini wakati huo watu wakilalamika, kuna wengine walikuwa na furaha kwa upande wao, hasa wazalishaji na wakulima wa miwa, kwa sababu walikuwa wanapata faida kubwa. Sasa, kama serikali ikisema ishushe bei kuwafurahisha wanunuzi, wauzaji na wakulima wa miwa watakuwaje? Kumbe kubalansi asili (balance of nature) ni muhimu sana.

Wakati hutaki kitu fulani kwenye maisha yako, kuna mtu anakitaka. Wakati ambao haupendi kitu fulani, kuna mtu anakipenda. Maisha yetu yako kwenye mitazamo na matamanio tofauti tofauti ili tutegemeane wote. Hapo ndipo

utakapoelewa hekima ya MUNGU ilivyo kubwa kwenye uumbaji wa ulimwengu.

Ukija ukiisogelea nafasi ya MUNGU, utaelewa jinsi ilivyo ngumu sana kubalansi asili. Yaani huyu ambaye haitaki mvua na huyu anayeitaka mvua wote waridhike na kumshukuru MUNGU. Nimekuja kugundua kuna hekima kubwa sana MUNGU aliyoitumia kuumba ulimwengu na jinsi ya kubalansi asili; hakuna mwanadamu aneweza kuwa na hekima hiyo. Ndiyo maana MUNGU akaweka majira mbalimbali kumbeba kila mtu na hali aliyonayo. Mfano: masika ni kipindi cha wakulima kufurahi sana kwa sababu ndipo wanapopanda mazao yao, lakini kiangazi ni kwa ajili ya wafanyabiashara na msimu wa mavuno pia. Wakati wa mavuno, wakulima huomba mvua isiwepo kabisa maana itaharibu mazao yao.

Kama ambavyo swala anategemea nyasi ili aishi, simba anamtegemea swala ili aishi, na nyasi zinategemea wote wawili wafe ili waoze na kuwa mbolea ya nyasi kustawi. Huo mzunguko ndio unaokamilisha ustawi na urari wa asili (balance of nature).

**Usichokihitaji Kinahitajika Kwa Wengine**

Kuna siku nilisafiri kwenda mkoa fulani. Nilipofika, nikashangaa tunashukia stendi ambayo imewekwa mbali sana na mji—yaani kama kilomita saba hivi kutoka mjini. Nikawa nawaza kichwani: "Kwa nini waweke mbali sana na mji? Walikuwa na maana gani kuiweka huku?" Nikiwa nimekwazika sana na kuona kama serikali haikufikiria vizuri, nikaenda kuchukua bajaji pale na kulipa Shilingi 1,000 kwenda mjini. Wengine pia walikuwa wakipanda bodaboda na wengine bajaji.

Tukiwa njiani, nikamwuliza yule dereva wa bajaji: "Hivi kwa nini serikali waliamua kuweka stendi mbali sana na mji?"

Yule wa bajaji akaniambia: "Kwa hiyo kaka, ulitaka sisi tupate wapi riziki yetu? Kitendo cha stendi kuwa mbali na mji ndiyo fursa ya sisi wenye bajaji na bodaboda kujipatia riziki." Akamalizia kwa kusema: "Maisha ni kutegemeana kaka. MUNGU kagawa riziki kwa makundi mbalimbali na wote tunategemeana sana ili kuishi."

Ndipo ujumbe wa balance of nature ulianza kuzunguka kichwani mwangu. Nilielewa kwa nini serikali iliweka stendi mbali na mji; kitendo cha kuwa mbali kinatengeneza mzunguko mkubwa wa uchumi. Bodaboda na bajaji watapata riziki zao, na kutoka kwenye hicho kipato watalipa kodi za serikali na tozo

mbalimbali kama ushuru. Lakini pia yatafunguliwa maduka mbalimbali ambayo yanasaidia wanaosafiri kupata huduma karibu badala ya kwenda mjini, na wengine wataajiriwa kufanya usafi na kujipatia riziki. Hii ndiyo maana halisi ya balance of nature.

**Nguvu ya Pamoja: Jinsi ya Kuthamini Utegemeano Huu**

Ili kufanikiwa, tunapaswa kujifunza kuheshimu umuhimu wa kila mtu kwenye huu mzunguko wa maisha. Hakuna anayejitosheleza:

Kama vile benki inavyokusanya fedha kidogo kidogo kutoka kwa watu wengi ili kutengeneza mtaji mkubwa unaozalisha faida, ndivyo na maisha yanavyohitaji mchango wa kila sekta ili uchumi usimame.

Kila mtu anayeonekana mdogo ana nafasi kubwa ya kukusaidia pale unapokwama. Thamani ya

mbeba mizigo, msafishaji, au dereva ni kubwa sawa na ya mtendaji mkuu.

Wakati mambo yako yanapochelewa kwa sababu ya "mvua" ya mtu mwingine, jifunze kusubiri kwa subira ukijua kuwa mzunguko wa asili ukigeuka, wakati wako wa kufaidika na "kiangazi" utafika pia.

## SURA YA TANO: MUNGU HAWEZI KUKUNYIMA VYOTE

Tukiwa tunasoma shule ya msingi, tulikuwa tunatoka sehemu ambayo ni kijijini sana. Hakuna umeme, hakuna maji. Tulikuwa tunatembea kwa miguu umbali wa kilomita 8 kwenda na kilomita 8 kurudi, jumla kilomita kumi na sita. Shati lilikuwa halina thamani kivile, limefubaa. Mguuni hakuna kiatu, na daftari zimekunjamana kupita maelezo.

Ukifika shule, unakutana na watoto wa matajiri wanaotunzwa kila siku. Wanavaa kaptula safi na shati jeupe linang'aa kila siku; wanapendeza sana kimwonekano. Wanakuja shule na hela ya kula vitumbua. Kipindi hicho kitumbua kinauzwa Shilingi 50 tu, lakini unakuta muda huo huna chochote mfukoni na wala nyumbani

hawakupi kitu chochote, zaidi ya kubeba kiporo cha viazi vitamu, tena vya baridi.

Lakini maajabu ya Musa; mkifika kwenye kitabu, wale watoto wa mabosi hawaoni ndani! Yaani kila pepa upo juu yao. Mwalimu akitoa zoezi, dakika tano ni nyingi umemaliza na kupeleka kusahihisha, hapo wengine wanahangaika kusolve hayo maswali. Kimwonekano walikuwa wasafi, lakini darasani madaftari yao yalikuwa machafu kwa makosa mengi sana. Hivyo, ilibidi wakutafute wewe uwaelekeze. Na ili wajenge ukaribu na wewe, itabidi kila siku wawe na zamu ya kukunulia vitumbua. Kwa hiyo, hata kama huna pesa, lakini vitumbua utakula!

Wao wana pesa lakini hawana uwezo mkubwa darasani, na mimi niliye mnyonge sina pesa lakini MUNGU kanipa uwezo mkubwa darasani.

Hii ndiyo maana halisi ya urari wa asili (balance of nature). MUNGU hawezi kukunyima vyote. Akikunyima pesa, atakupa akili ya kusaidia wengine na wao watakupa kile usichoweza kukipata kwa wakati huo. Ndio maana hata mtaani kuna watu hawajasoma lakini wameajiri wasomi kufanya vitu ambavyo wao wenyewe hawawezi kuvifanya.

Ndio maana nikasema, MUNGU hakupi vyote, lakini pia MUNGU hakunyimi vyote. Lazima atakupa kimoja wapo tu ili kupitia hicho kitu upate riziki yako ya kila siku. Ubaya unaanza pale ukijiona unaweza kuishi bila msaada wa mtu mwingine; ndipo utakapouona ugumu wa maisha. Lakini ukitambua uwepo wa watu wengine ili waweze kufanya kile ambacho huwezi kukifanya, utafanikiwa sana. Maana kinachoweza kufanywa na miguu, mikono

haiwezi kukifanya; na kinachofanywa na masikio, macho hayawezi kukifanya. Kila mtu kapewa sehemu yake ya utambulisho.

Ukisema hauna kitu kabisa cha kufanya ili ufanikiwe utakuwa muongo, maana kwenye balance of nature, MUNGU kampa kila mtu na kila kiumbe kitu cha kufanya ili kujipatia riziki. Ndio maana YESU alisema hata kunguru ambao hawapandi na wala hawavuni, lakini MUNGU huwalisha. Hii ni kwa sababu kwenye balance of nature, kila kitu kimepewa uwezo wa kujipatia riziki katika mazingira mbalimbali. MUNGU hawezi kukupa vyote, na MUNGU hawezi kukunyima vyote. Akikunyima pesa, atakupa akili ya kusaidia wengine waliofeli darasani, na wao atawapa pesa ili wakupe hizo pesa. Hiyo ndiyo balance of nature.

Hekima ya ajabu ni hii:

MUNGU hakunyimi vyote, bali anakupa kipawa cha kipekee. Ukikithamini na kukitumia kwa manufaa ya wengine, ndipo riziki na heshima zikitakufuata.

**(The Law of Divine Compensation)**

Ulimwengu hauna upendeleo na haujawahi kuacha pengo lisilozibwa. Unapoona umezaliwa katika mazingira duni yasiyo na mali wala fedha, usitazame mikono yako mitupu, bali tazama hazina iliyofichwa ndani ya kichwa au moyo wako. MUNGU anapofunga mlango wa utajiri wa kurithi, anafungua milango mamia ya ubunifu, ustahimilivu, na akili kali. Upungufu wa nje daima ni kichocheo cha utajiri wa ndani. Yale mapungufu uliyonayo leo ndio mtego wa kimungu unaowalazimisha wenye navyo kuja kwako kesho ili wapate suluhisho la maisha yao.

## Biashara ya Kubadilishana Mapungufu (Trading Our Deficits)

Maisha ni soko kubwa ambapo hatuuzi vitu tulivyonavyo tu, bali tunabadilishana mapungufu yetu ili kukamilishana. Hakuna binadamu aliyeumbwa kama kisiwa kinachojitosheleza. Tajiri anapompa maskini mshahara, na maskini anapompa tajiri nguvu au maarifa yake, wote wawili wanakuwa wametatua shida zao. Kiburi cha kufikiri una kila kitu ndicho chanzo cha kuanguka kwa wanadamu wengi. Unapogundua kuwa kile usichonacho kipo kwa mwenzako, unaacha dharau na unaanza kujenga madaraja ya ushirikiano badala ya kuta za utengano.

. Siri ya Kunguru na Maisha ya Imani

Kama ndege wa angani wasio na maghala ya kuhifadhia chakula wanavyoamka asubuhi wakiwa na uhakika wa kushiba, ndivyo

mwanadamu anavyopaswa kutembea kwa ujasiri akijua kuwa ana thamani kubwa. Kipaji ulichonacho, hata kiwe kidogo kiasi gani machoni pa watu, ni "leseni" yako ya kupata riziki hapa duniani. Shida sio kutokuwa na pesa, shida ni kutokutambua kile ulichopewa bure na Ulimwengu. Ukiamsha uwezo uliolala ndani yako, mazingira magumu uliyopo sasa yatageuka kuwa uwanja wako wa ushindi na shuhuda kubwa.

Nguo safi na viatu vya thamani vinaweza kusafisha mwili wa nje, lakini haviwezi kuongeza uwezo wa akili iliyolala. Thamani ya kweli ya mwanadamu haipimwi kwa kile alichovaa mwilini mwake, bali kwa kile anachoweza kutoa kichwani na moyoni mwake ili kuifanya dunia iwe mahali bora. Watoto wa matajiri walihitaji viazi vyetu vya baridi na akili

yetu ili kufaulu, na sisi tulihitaji fursa zao ili kusonga mbele. Usijidharau kwa sababu ya udogo wa mwanzo wako; kumbuka kuwa dhahabu safi kabisa haipatikani kwenye maduka ya kifahari, bali huchimbwa chini kabisa ya ardhi chafu na yenye matope.

## SURA YA SITA: WATU WOTE HATUWEZI KUFANIKIWA WOTE KWA SIKU MOJA

### -Chanzo Cha Ugumu Wa Maisha Ni Ubinafsi

Kwenye utafiti niliofanya kwa muda mrefu sana hapa duniani, nimekuja kugundua kitu kimoja. Wakati mtu anahangaika apate wapi pesa ya kodi, chakula, au ada ya watoto, kuna mtu mwingine ana pesa ya kutosha sana kiasi cha kukosa mahali pa kuipeleka. Lakini, hawezi kumpa mtu bila kuwepo na mabadilishano ya thamani (exchange of value). Kwenye maisha halisi, hakuna mtu anayeweza kutoa pesa zake kwa mtu mwingine kama huyo mtu hajachangia kitu chochote kwake. Ndiyo maana halisi ya msemo wa "hakuna pesa ya bure", au wenzetu wazungu wanasema, "No free lunch in America."

Nilikuja kugundua kuwa, wakati kuna mtu anawaza apate wapi ajira ili ajipatie walau riziki kidogo ya kila siku, kuna mwingine anachukua Shilingi milioni 350 anaenda kununua gari la kutembelea. Mwingine anaenda kununua cheni za kuvaa shingoni. Kumbe, hiyo milioni 350 angewekeza kwenye kampuni ya usambazaji wa bidhaa, kuanzisha biashara mbalimbali, au kiwanda cha kusindika bidhaa fulani, angeweza kutengeneza ajira kwa zaidi ya watu 300.

Sasa, kama kila mtu aliyejaliwa na MUNGU kuwa na utajiri mkubwa angekuwa na wazo kama hilo, hakika kusingekuwa na uhaba wa ajira. Ugumu wa maisha usingekuwepo kabisa. Lakini, ubinafsi wa watu wengi ndio umesababisha ugumu wa maisha kwa watu wengi.

Nilichokuja kugundua kwenye maisha ni kwamba, hatuishi kwa ajili yetu wenyewe bali kwa ajili ya watu wengine. Yaani, mafanikio yako si yako peke yako. Kiuhalisia, ni ya watu wengi sana walio nyuma yako. Lakini ubinafsi hutufanya kuona kama kila tunachomiliki ni chetu peke yetu.

Kuna kipindi watu waliamua kuishi maisha ya ujamaa na kushiriki kila kitu. Matendo ya Mitume 4:32, 34 (Biblia Takatifu) inasema: “Na jamii ya watu walioamini walikuwa na moyo mmoja na roho moja; wala hapana mmoja aliyesema ya kuwa kitu cho chote alicho nacho ni mali yake mwenyewe; bali walikuwa na vitu vyote shirika. Wala hapakuwa na mtu mmoja miongoni mwao mwenye mahitaji; kwa sababu watu wote waliokuwa na viwanja au nyumba

waliviuza, wakaileta thamani ya vitu vile vilivyouzwa."

Kipindi kile cha ujamaa, watu wote walishiriki kila kitu na hakuna kilichopungua kwa sababu walishare wote. Kila mtu akawa na amani. Hapakua na maskini wala tajiri aliyempita mwenzake kwa mbali, maana wenye mafanikio waliwasaidia wale wasio na mafanikio na kuwavuta juu.lakini watu walipoongezeka zaidi ubinafsi ulianza na kuanza kwa mataba ya Tajiri na maskini msomi na asiye soma, japokuwa mtindo huu wa maisha SIYO mzuri Sana kama unayatazama maisha kwa jicho la tatu.

## Watu Wote Hatuwezi Kufanikiwa Kwa Siku Moja

Kuna watu wengi sana huwa wanahamasisha watu kujiajiri wao wenyewe. Wengine wanasema ajira ni utumwa. Wengine wanasema

huwezi kuwa tajiri kwa kutegemea ajira. Wengine hudai mshahara ni kama madawa ya kulevya yanayokufanya usahau ndoto zako. Ni ukweli kabisa kwamba mtu hawezi kufanikiwa kwa mshahara pekee, na ajira inaweza kuwa utumwa. Na hata Mimi naunga mkono hoja hiyo Lakini swali la kujiuliza: Je, wote tukiwa matajiri na mabosi, nani angekuwa mfanyakazi wa mwenzake?

Je, ulishawahi kujiuliza kama pasingekuwepo walimu wa shule za msingi, sekondari, na vyuo (ambao ni waajiriwa), watu wangefundishwa na nani? Hata wewe unayesema ajira ni utumwa, ungesomea wapi na ungefundishwa na nani? Jibu ni kwamba, kuna vitu vingine ni MUNGU pekee anayejua namna ya kuvibalansi; mwanadamu huwezi.

Kama MUNGU kakujalia kuwa na kampuni yako binafsi na unatengeneza pesa nyingi sana, mshukuru MUNGU kwa ajili ya hilo. Lakini usiwadharau wengine pia, maana nao wapo kwenye foleni. Kulingana na urari wa asili (balance of nature), zamu yao ya kuwa juu itafika tu. Hatuwezi kufanikiwa wote kwa siku moja. MUNGU ni fundi; anajua namna binadamu tunavyotegemeana. Ndiyo maana katugawanyia kila mtu kipande chake na jukumu (assignment) lake la kufanya. Kila mtu atafanikiwa kwa wakati wake kwenye kusudi lake tukiwa hai hapa duniani.

Wanafunzi shuleni hawawezi kumaliza wote kwa siku moja. Lazima watofautiane miaka. Hawa wako kidato cha nne, wengine ndio wanaanza kidato cha kwanza. Hawa wako chuo kikuu, wengine wanaingia ngazi ya juu ya

sekondari (advance). Kama ambavyo haitatokea siku moja wanafunzi wote shuleni wamalize masomo kwa siku moja, ndivyo ambavyo hakuna siku watu wote tutafanikiwa kwa siku moja ili kila mtu awe juu. Hii ndiyo hekima ya MUNGU na urari wa kimungu wa asili (divine balance of nature).

Hata kwa vijana ambao bado hamna ajira wala kazi maalum ya kufanya na mnaunga-unga tu, habari njema ni kwamba siku yenu yaja. Nawe utafanikiwa sana kwa wakati wako. MUNGU amefanya kila kitu kizuri kwa wakati wake. Acha wengine waitimu leo na washerehekee mahafali yao, lakini ipo siku na wewe utavaa joho na kusherehekea siku ya kuhitimu kwako kwenye shule ya uzima (school of life).

Uchungu wa maisha huanza pale tunapoanza kujilinganisha na wengine tukidhani karatasi

zetu za mitihani ni sawa. Kumbe tunaweza kuwa kwenye chumba kimoja cha mitihani, tukitumia aina moja ya kalamu na msimamizi mmoja, ila tukawa na maswali tofauti kabisa! Hivyo, majibu yetu lazima yawe tofauti na ufaulu wetu lazima utofautiane. Hakuna kitu kinachokosesha raha kama kujilinganisha na wengine. Kila unapochukua nywila (password) ya mtu mwingine kujaribu kuingia kwenye akaunti yako, lazima ikugomee tu. Akaunti yako inahitaji password yako mwenyewe na sio ya jirani yako. Hivyo ndivyo ilivyo unapojilinganisha na wengine.

## Hakuna Kitu Kinakosesha Raha Kama Kujilinganisha Na Wengine

Kuna siku nilienda kijijini nilikosomea shule ya msingi. Nikakutana na vijana wenzangu niliosoma nao darasa la saba. Wao walifeli

darasani na mimi nikafaulu na kuendelea hadi chuo kikuu. Kitu kikubwa nilichoona kwao ni kwamba wamefanikiwa kiasi chake; wamejenga nyumba, wana pikipiki, na wengine wana mashamba. Mimi mwaka huo ndio nilikuwa nimemaliza chuo na kurudi mtaani. Wakawa wanasema: "Yani elimu ya Tanzania siyo nzuri kabisa. Ona huyu kasoma miaka mingi zaidi shuleni na sasa hivi hana kitu, halafu hawa waliokomea la saba wana hatua kwenye maisha, wana maduka, pikipiki, mashamba, na nyumba."

Niliposikia hayo, moyo uliuma sana. Nikawa nawaza kichwani kuwa kuna ukweli ndani yake. Ona kweli sasa hivi mimi ndio naanza upya, ila hawa wenzangu tayari wana hatua kadhaa mbele, mimi hata ajira yenyewe bado. Lakini nilipokaa na kutafakari kwa kina, nikajua kuwa ni swala la muda tu. Kama MUNGU akiamua

kuniinua, ni ndani ya siku moja tu na kuwa juu yao wote, na wao wanakuwa watumishi wangu. Maana nafasi niliyopo naweza kuwa mkurugenzi wa sekta yoyote, naweza kuwa afisa madini, au mtu yeyote mkubwa kwa wakati wowote. Kozi niliyosomea mimi, hata ukisema uajiriwe tu, unakuta mshahara wake ukiwa unaanza ni Shilingi milioni tatu, tofauti na marupurupu (bonus) zingine.

Ukiachana na ajira, thamani yangu kwenye maisha halisi ni kubwa sana kuliko ya mtu aliyekomea darasa la saba. Pesa sio makaratasi, bali thamani uliyonayo ndio pesa. Na kweli, baada ya muda, nilipoanza kuandika vitabu vyangu na kuuza, nilianza kuingiza kipato kikubwa sana nikiwa nimekaa tu nyumbani. Wakati mwingine nikiwa nimelala, watu wanatuma mihamala tu. Wakati huo, wenzangu

wa darasa la saba lazima waende shambani kulima na kusubiri mwaka mzima ili waweze kupata kipato kikubwa—yaani msimu ukiisha hadi mwakani tena. Wakati huo mimi nikiandika kitabu kimoja tu, ninaweza kula kwa miaka mingi. Wakati huo Mimi ni sawa na wateule wakuwania nafasi yoyote Ile kubwa kwenye inchi hii MUNGU akiamua ,maana ninayo maandalizi.

Nikagundua kujilinganisha ni kitendo cha kujipunguzia thamani uliyonayo. Ndio maana kila unapojilinganisha, unajiona mnyonge na unazidi kupungua kila siku. Katika balance of nature, kila mtu atafanikiwa kwa wakati wake na kwenye kusudi lake.

Wote tukiwa wafanyabiashara, wote matajiri, wote waajiriwa, wote wakulima, au wote watumishi wa umma, nani atamtegemea

mwenzake? MUNGU ana hekima inayopita kiwango cha elimu ya wanadamu. Ndio maana alisema mawazo yake yako juu sana kuliko mawazo yetu wanadamu, wala njia zake ziko juu sana kupita njia za wanadamu wote.

**Fumbo la Makao ya Mbegu ardhini**

Hekima ya asili inatufundisha kuwa, kitendo Cha kufunikwa na udongo hakuna maana ya kuzikwa ili upotee, bali ni kuandaliwa ili uote. Vijana wengi waliopo mtaani leo wanajiona wamepotea kwa sababu wapo gizani, wakidhani wenzao waliotangulia kufanikiwa wamewashinda. Lakini ukweli ni kwamba, kila mbegu ina msimu wake wa kukaa ardhini kabla ya kuchomoza na kuwa mti mkubwa unaozaa matunda. Usihuzunike unapoona wengine wanavuna matunda yao sasa; tulia gizani

ukichaa mizizi, kwani kuchomoza kwako kutashangaza dunia.

**Thamani ya Msingi Usioonekana kwa Macho**

Katika majumba makubwa ya kifahari tunayoyaona mijini, sehemu yenye nguvu na iliyobeba uzito wote ni msingi uliopo chini ya ardhi, ambao hakuna mtu anayeiona wala kuisifia. Waajiriwa wa ngazi za chini, walimu, na mafundi ndio msingi thabiti unaoshikilia ghorofa la uchumi wa nchi na utajiri wa matajiri wakubwa. Ubinafsi hutufanya tusifu rangi za kuta na madirisha ya vioo juu, tukisahau kuwa bila uimara wa ule msingi uliosimama gizani, jengo zima lingeanguka. Kila mmoja wetu, iwe bosi au mfanyakazi, ana umuhimu wa msingi usiopaswa kudharauliwa.

Tofauti za vipato na vyeo hapa duniani sio alama ya kuwa wengine ni bora kuliko wengine, bali ni

mfumo wa kutoshelezana ili dunia isisimame. Tajiri anahitaji akili na nguvu ya maskini ili kulinda na kukuza mali zake, na maskini anahitaji maono na mtaji wa tajiri ili kupata mkate wake wa kila siku. Hakuna aliye juu ya mwingine kiuhalisia; sote ni vipande vya fumbo kubwa la picha (puzzle) ambalo haliwezi kukamilika kama kipande kimoja kikikosekana. Unapomnyanyasa mnyonge, unajikata ulimi wako mwenyewe, kwani yeye ndiye anayebeba sauti ya kesho yako.

**Siri ya Nyakati na Password ya Mafanikio**

Kila mwanadamu amezaliwa na namba ya siri (pin code) ya maisha yake inayofungua milango ya baraka zake kwa sekunde yake maalum iliyopangwa na ulimwengu. Kosa kubwa tunalofanya ni kujaribu kulazimisha nywila za wenzetu zifungue kufuli zetu, jambo linaloishia

kutufungia nje ya hatuzi zetu wenyewe. Kuona mwenzako amenunua gari au amejenga akiwa na umri mdogo kusikufanye uhisi umefeli mtihani wa maisha. Tulia kwenye mstari wako, jenga thamani yako ya ndani, kwani mfumo wa asili haujawahi kukosea kutoa majibu sahihi kwa mtu aliyesubiri majira yake kwa subira na kazi ya bidii.

## SURA YA SABA: NGA'TA UNACHOWEZA KUTAFUNA

Kaka mmoja ambaye alizaliwa kwenye maisha ya kawaida, kwao hakuna pesa za kutosha, alikuwa na mahusiano na mdada mmoja ambaye wazazi wake walikuwa na uwezo mkubwa sana kiuchumi. Wawili hawa walikutana chuoni wakiwa masomoni. Yule binti baba yake mzazi alikuwa Marekani anafanya kazi, na mama yake alikuwa kwenye taasisi za serikali kama afisa masoko, akizunguka mikoa mbalimbali nchini Tanzania na akilipwa mshahara mzuri sana. Huku wazazi wa kijana wa kiume wakiwa ni wakulima wote na wala hawana chanzo kingine cha mapato tofauti na kilimo.

Mahusiano yao hawa watu wawili yalienda kwa muda lakini baadaye changamoto zilianza. Ni kweli walikuwa wanapendana sana, lakini

ukweli mchungu ni kwamba walikuwa hawaendani. Naposema kuendana simaanishi kwenye maumbile au kimwonekano, bali ile hadhi ya kimaisha. Kama nilivyosema, watu wote ni sawa mbele za Mungu lakini siyo sawa kwenye uso wa nchi. Kwa hiyo, kuna muda hawa watu wawili walikuwa wanapeana zawadi; mkaka anaishia kumnunulia juisi na bites tu, wakati huo mdada alikuwa anaweza kumnunulia saa za gharama, notebook, na viatu vya gharama kubwa kwa sababu yeye alikuwa anapewa na wazazi wake fedha nyingi sana. Akitumiwa na baba yake leo, kesho mama yake anatuma pia, lakini pia alikuwa na mkopo wa serikali (boom). Wakati huo mkaka, japokuwa alikuwa na mkopo huo, mkopo alikuwa anautumia kulipia ada ya chuo na kuwatumia wazazi wake nyumbani wakiwa wamekwama. Pia kulikuwa na mdogo wake anasoma, kwa hiyo lazima amtumie pocket

money shuleni. Unaweza kuelewa jinsi ambavyo alikuwa na wakati mgumu sana kwenye swala zima la kubalance uchumi wake kiasi cha kupata hela ya kumzawadia mpenzi wake.

Walienda kwa muda, baadaye huyu dada akaanza kuona kama kaka hampendi maana yeye anajitoa sana lakini mwamba anaishia kumpa zawadi za kitoto tu. Hakujua kijana anapitia nini hasa, kama ilivyo kawaida ya wanaume wengi huwa hawapendi kuonyesha udhaifu mbele ya mwanamke; hata kama kuna kitu kinawala ndani kwa ndani watajikaza tu. Kwa hiyo, hakuwahi kumwambia kuwa yeye ndiyo tegemezi kwenye familia yake. Dada alihisi kabisa huyo kaka hampendi na yupo tu kwenye mahusiano kusukuma siku za kuishi chuoni wamalize masomo basi, ingawa yule kaka kweli alikuwa amemwahidi atamuoa binti yule na alikuwa

anampenda sana. Lakini hakuna jinsi, maana upendo hauwezi kuzidi kanuni. Nature ikawapeleka kutokuelewana baina yao. Nia na shauku ya kujitoa kwa ajili ya mchumba wake yule kaka alikuwa nayo, lakini according to the balance of nature, huwezi kutoa usichokuwa nacho. Kanuni inasema unatoa kwenye kingi na sio kutoa kwenye vichache, utapata deni, hata maandiko yakasema katika 2 Wakorintho 8:12-14 (Biblia Takatifu): "Maana, kama nia ipo, hukubaliwa kwa kadiri ya alivyo navyo mtu, si kwa kadiri ya asivyo navyo. Maana sisemi hayo, ili wengine wapate raha nanyi mpate dhiki." Kumbe mtu anaweza kuwa na nia ya kutoa lakini sasa mazingira yakamzuia kabisa asiweze maana hana uwezo huo. Kwenye maisha ni muhimu sana kufahamu kuwa unatakiwa kung'ata unachoweza kutafuna, na sio

kulazimisha kubugia sahani nzima halafu ukashindwa kumeza.

Mahusiano ya watu hawa yalikwama yakaishia njiani. Nadhani kaka alihuzunika sana na yule dada pia, na pengine kuona kama kuna usaliti na kadhalika. Lakini hebu chukua picha kama hawa watu wangefika kwenye hatua ya ndoa; je, huyu kaka angekubalika ukweni? Hata kama atakubaliwa, je, angeweza kumudu mahari ya huyo dada? Maana tuta la viazi kwa sisimizi ni mlima mrefu lakini kwa binadamu ni mwinuko mdogo tu. Kama kaka huyu angeambiwa mahari milioni tano, huku kwenye maisha yake yote hajawahi kuipata hiyo fedha, angejisikiaje? Hata kama wanesema mahari anayoweza kumudu, je, gharama ya kuendesha harusi ukumbini angemudu? Kumbuka ni mtoto wa mtu mzito anayeolewa. Tuseme gharama zote apewe

ukweni? Je, yeye mwenyewe angeweza kuishi na huyo binti wa kitajiri kwenye maisha ya kilimo ikiwa mtoto wa watu amezoea kukaa geti kali? Utakuja kuelewa kuwa kaka huyu, hata kama angeishi na binti huyo, maisha yao yangekuwa na mishikemishike mingi maana hawako compatible. Ndiyo maana Mungu akasema nitakufanyia msaidizi wa kufanana naye; alikuwa anafahamu kuhusu matabaka tuliyonayo wanadamu. Ndugu wanaume wenzangu, natoa ushauri wa hekima kwa vijana wenzangu: ukiwa unataka kucheza mechi ya mpira wa miguu kwa dakika zote tisini, jitahidi sana uvae kiatu cha saizi yako kinachokuenea vizuri, sio kila kiatu unaweza kuvaa. Kisipokuenea hutakuwa comfortable kwenye mchezo na pengine usiweze kumaliza dakika zote tisini kwenye mchezo. (Namaanisha jitahidi kuoa mwanamke unayeweza kumudu kumtunza,

msije kukomea njiani). Ng'ata unachoweza kutafuna na sio kulazimisha kubugia sahani nzima halafu ukashindwa kumeza. Watu wako kwenye viwango na maisha yako kwenye viwango, angalia kiwango chako kwanza kabla hujakaribisha mtu kwenye maisha yako.

**Nga'ta Unachoweza Kutafuna**

Katika safari ya kuitafuta madhabahu ya ndoa, mwanamume lazima afahamu kuwa heshima ya nyumba haijengwi kwa hisia za mapenzi pekee, bali inasimamiwa na uwezo wa kiuchumi na utulivu wa kisaikolojia. Unapomchagua mwenzi wa maisha, unapaswa kuangalia mbali zaidi ya uzuri wa sura au tabasamu lake la sasa; tazama ikiwa asili ya maisha yake na matarajio yake vinaoana na uhalisia wa mifuko yako na majukumu ya familia yako. Mwanamume anayejilazimisha kuingia kwenye matabaka

makubwa yaliyomzidi kimo, anajisajili kwenye utumwa wa nafsi ambapo kila siku itakuwa ni mtihani wa kutaka kuthibitisha thubutu yake, jambo linaloweza kumfanya apoteze utu na mwelekeo wake wa kimaisha. Hekima inakutaka utafute mtu ambaye mnaweza kuanza naye chini mkapanda pamoja, au mtu aliye tayari kushuka na kukaa kwenye viwango vyako vya sasa ili mbebe jembe kwa pamoja kuelekea kesho yenu.

Hali kadhalika, utambuzi wa viwango vyako vya kimaisha haumaanishi kuwa wewe una mapungufu au unajidharau, bali ni ishara ya ukomavu wa hali ya juu na nidhamu ya kimaono. Ukweli ni kwamba, mwanamke aliyezoea maisha ya kifahari tangu utotoni anahitaji gharama fulani ili kuendeleza furaha na amani yake ya ndani, na ikiwa huna uwezo wa kumpatia mazingira hayo, hata kama

anakupenda, baada ya muda mrefu uhalisia wa upungufu utaanza kuzua nyufa kwenye ndoa yenu. Mapenzi yanaweza kuvumilia njaa kwa usiku mmoja chuoni, lakini hayawezi kuvumilia bili za maji, umeme, kodi ya nyumba, na ada za shule za watoto huko mbeleni. Kuoa mwanamke anayeendana na saizi yako ya kiuchumi kunakupa amani ya akili na nafasi ya kupanga mikakati ya ukuaji bila kuwa na shinikizo la madeni au hofu ya kudharauliwa mbele ya wakwe zako.

Mwisho kabisa, fumbo la msaidizi wa kufanana naye halipo kwenye kufanana kwa majina au makabila, bali lipo kwenye ulinganifu wa maono, mitazamo, na uwezo wa kubeba changamoto kwa pamoja. Mwanamume mwenye busara haongozwi na sifa za nje au presha ya marafiki, bali hukaa chini na kupiga hesabu za

gharama ya ujenzi kabla ya kuweka msingi wa nyumba yake. Tafuta mwanamke ambaye zawadi yako ya dhati—hata iwe ndogo kiasi gani—itakuwa na thamani kubwa moyoni mwake kwa sababu anatambua jasho na mzigo uliopo nyuma ya mikono yako. Jenga maisha yako kwanza, jua mipaka na uwezo wako, na kisha chagua mshirika ambaye kiatu chake cha maisha kinalingana na hatua zako, ili kwa pamoja muweze kukimbia mechi hii ya maisha kwa ushindi na bila majeraha hadi dakika ya tisini.

## SURA YA NANE: MWENYE NGUVU MWITE BINGWA

Kuna siku nilikuwa nimepanda bajaji, tukafika sehemu ambayo kulikuwa na semi inakatisha barabara. Magari yote yalikuwa yamesimama, na pikipiki zote zimesimama kabisa. Kichwani nikawaza: semi moja imesababisha kila aina ya chombo cha moto kusimama. Lilipomaliza kukatisha barabara, magari na vyombo vingine vikaendelea na safari.

Nikiwa natafakari, nikaona pia mwenye pikipiki alikuwa akimpisha mwenye gari la mizigo, na mwenye gari la mizigo akimpisha mwenye semi. Baadaye Roho wa hekima akaanza kuniambia maneno haya:

Kwenye maisha tunaachana uwezo na nafasi. Kama ambavyo unaona semi likiwa linakatisha

basi magari yote na vyombo vingine vinasimama, ndivyo ilivyo kwenye maisha—watu wote si sawa. Kuna watu wanaostahili heshima; wakiwa wanapita huna budi kusimama na kuacha wapite kwanza, na wewe utaendelea na safari baadaye. Kama ambavyo mtembea kwa miguu humpisha mwendesha baiskeli, na wa baiskeli humpisha wa pikipiki, wa pikipiki humpisha wa gari, na mwenye gari lazima ampishe mwenye semi—ndivyo maisha yetu yalivyo. Binadamu wote sio sawa, hawafanani, lazima kuheshimu kila nafasi ya mtu.

Ndipo nilianza kuelewa kwa nini kwenye msafara wa rais magari mengine lazima yasimame mpaka atakapopita. Ndipo nilianza kuelewa kwa nini mfalme au rais wa nchi akiwa anapita watu lazima wasimame. Mwanzo nilidhani ni kuabudu mtu au cheo, kumbe

hapana, bali ni kile alichosema Paulo: Mpeni kila mtu nafasi na heshima anayostahili. Kama ni heshima basi apewe heshima, kama ni kunyenyekewa basi apewe kunyenyekewa.(Warumi 13:1_8)

Hakika mwenye nguvu mwite bingwa. Kuna watu wanaostahili heshima kwa sababu ya nafasi walizo nazo, kwa hiyo lazima tuwape heshima. Kauli ya kusema binadamu wote ni sawa ni kuonyesha kiburi tu. Tupo sawa mbele za Mungu, lakini siyo kwenye uso wa nchi. Hapa duniani kila mtu ana nafasi yake aliyopewa, na tunatofautiana kila mmoja na sehemu aliyopewa. Kama vyombo vya moto vinaheshimiana, je binadamu hawawezi?

Tofauti yetu na vyombo vya moto ni kwamba sisi tuna nafasi ya kukua na kufika hatua ya kuheshimika. Siyo kama bajaji ikitengenezwa

haiwezi kuwa gari, au baiskeli haiwezi kuwa pikipiki tena. Lakini sisi binadamu tunaweza kuwa chini, na baada ya muda tukawa juu. Nafasi ya kuheshimika na kufanikiwa kuwa mtu mkuu ipo kwa kila mtu. Utofauti unakuja kwenye maarifa uliyonayo na juhudi binafsi. Siyo kama bajaji ikitengenezwa itabaki kuwa bajaji milele, au pikipiki haiwezi kuwa gari hata siku moja. Lakini sisi binadamu tunapaswa kuheshimiana kila mmoja kulingana na nafasi aliyo nayo, kuwaheshimu waliokutangulia na walio na vyeo huku ukiamini kwamba nawe unafata pia. Ndiyo maana halisi ya msemo wa mwenye nguvu mwite bingwa. Hii ndiyo maana ya balance of nature: tupo sawa mbele za Mungu, lakini siyo sawa duniani.

(Nguvu ya Itifaki na Mamlaka):

Utawala Bora Huheshimu Alama za Mamlaka: Wafalme na viongozi wakuu hawaombi heshima, bali itifaki ya uwepo wao inalazimisha mazingira kujipanga yenyewe. Kiongozi mwenye hekima anatambua kuwa unyenyekevu mbele ya wenye mamlaka makubwa zaidi sio udhaifu, bali ni ukomavu wa kiakili na kisheria unaolinda amani ya nchi.

Ufalme wa kweli hauji kwa kelele bali kwa uzito wa maamuzi yako. Kama vile semi inavyosimamisha barabara bila kutumia nguvu nyingi, kiongozi mkuu anapaswa kuwa na uzito wa kimkakati unaofanya soko, uchumi, na mifumo kumsikiliza pindi anapotoa amri.

Simba hawezi kuwa mfalme wa mwitu ikiwa atadharau utaratibu wa anga na ardhi. Kiongozi mkuu ana wajibu wa kuheshimu na kulinda haki za walio chini yake (nyasi na swala), kwa

sababu bila utulivu wao, hakuna barabara salama kwa semi kupita.

**Ng'ata Unachoweza Kutafuna**

Siku moja tembo walikuwa wanatembea kwenda sehemu moja. Walitumia dakika tano tu wakawa wamefika walikopenda. Wakaja swala, wakatumia dakika thelathini na tano kuvuka eneo hilo. Mahali ambapo tembo walitumia dakika tano, swala walitumia dakika thelathini na tano—tofauti ya nusu saa kabisa.

Mtu mmoja aliyekuwa na wenzie kwenye utalii wa mbuga za wanyama akauliza: Kweli nimeamini kuna utofauti mkubwa sana kati ya tembo na swala. Mwingine akasema: Mtoto wa tembo aliyezaliwa leo ni mkubwa kuliko swala mzee. Mwingine akadakia: Hata paka mtoto ni mkubwa kuliko panya mzee. Wote wakacheka lakini ujumbe ni kwamba;

Maisha yako kwenye viwango; viumbe vyote haviko sawa kabisa hata watu pia hatuko sawa. Hatufanani kabisa kwenye maisha. Kwa mujibu wa balance of nature, kuna mapengo Mungu aliyoyaweka. Siyo kwamba alipendelea, la hasha, bali ili kuwe na usawa wa uumbaji. Kwa hiyo ni muhimu sana kung'ata unachoweza kutafuna na siyo kulazimisha kubugia sahani nzima ya chakula halafu ukashindwa kumeza.

Tuta la viazi kwa sisimizi ni mlima; litamchukua nusu saa kupanda na kushuka. Lakini kwa binadamu ni mwinuko mdogo wa ardhi ni kitendo cha kunyanyua mguu tu na kusonga mbele. Maisha yako kwenye viwango. Usilazimishe kiwango cha maisha ulichopo kilingane na wengine.

Kuna mtu anaweza kutumia milioni tano kwa siku kama matumizi ya kawaida, lakini

mwingine kipato chake cha mwaka mzima ndiyo hiyo milioni tano, na pengine haifiki. Huyu akilazimisha afanane na yule mwingine ambaye matumizi yake ya siku ni milioni tano, lazima ataumia. Ndiyo maana waswahili wakasema: Ukiiga kujisadia kwa tembo lazima uchanike msamba.

Balance of nature inatufundisha kuvumilia hali yako kwa muda, ukielewa kwamba muda utakuja ambapo na wewe utafika kwenye kiwango cha juu sana na kuweza kufanya unachokitaka.

Kuna watu wana nguvu za kiuchumi kama tembo—dakika tano tu zinawatosha kulipia bili ya kila kitu wanachokitaka. Lakini kuna wengine wanahitaji nusu saa, siku moja, wiki, miezi, na pengine miaka. Hatuko sawa kwenye maisha. Balance of nature inatufundisha kuelewa

mapungufu yetu na kuridhika kwa hatua aliyokupa Mungu, ukimwamini kwamba kuna mahali unaenda pia.

Kuna mtu anaweza kujenga nyumba nzuri sana kwa mwezi mmoja wakati huo kuna mtu ili ajenge atatumia miaka mitano au kumi, that is the difference, hatuko sawa kikubwa kila mtu atafanikiwa kwa wakati wake. Na kila mtu atakula kwa urefu wa kamba yake. hatuwezi kufanikiwa wote kwa siku Moja yani kila mtu awe juu usiku mmoja balance of nature itakua changamoto, hata mifumo ya nature haiwezi kuruhusu Hilo.

**(Usimamizi wa Rasilimali na Subira ya Kimkakati)**

Wafalme na wafanyabiashara wakubwa wanaelewa kuwa huwezi kuendesha vita au himaya kwa kutumia bajeti ya kuazima.

Kung'ata unachoweza kutafuna ni kanuni ya dhahabu ya ulinzi wa ukwasi (liquidity) na mtaji. Simba anayekimbiza kila swala bila kupima pumzi yake huishia kufa kwa njaa katikati ya savana.

Kiongozi mwenye maono haharakishi matokeo; anajua kuwa mtoto wa tembo bado anahitaji kulindwa na mama yake kabla ya kuangusha miti mikubwa. Kuridhika na hatua ya sasa huku ukiandaa miundombinu ya hatua inayofuata ndiyo siri ya ufalme unaodumu vizazi na vizazi.

Kiongozi anayelazimisha kuonekana kama 'Tembo' wakati uwezo wake wa sasa kiuchumi ni wa 'Swala' anajiandaa kuanguka. Wafalme wa kweli hujenga misingi imara chini ya ardhi kabla ya kuonyesha fahari ya maghorofa yao juu ya nchi, wakitambua kuwa urefu wa kamba yao ndiyo unaoamua usalama wa mifugo yao.

## SURA YA TISA: UNACHOKITUNZA KITAKUTUNZA PIA

**kanuni ya Kupokea kwa Kutoa (The Law of Reciprocity)**

Tukiwa kijijini tulikua wafungaji na wakulima pia , kila siku asubuhi tulikua tunaenda kuwachunga ng'ombe malishoni ,siku wakishiba vizuri sana jioni yake walikua wakitoa maziwa mengi Sana, lakini wasiposhiba vizuri walikua wakitoa maziwa kidogo Sana kiasi Cha kutowatosha wote kwenye familia. Lakini pia tulipotaka kuwauza ilibidi tuwachunge vizuri na kuwalisha pupa za kutosha tukichanganya na chunvi ili wanenepe , ukija kumpeleka mnadani ananunuliwa kwa Bei ya juu sana Hadi na wewe mfungaji unafurahia lakini ukiwaacha wakonde Wala huwatunzi walikua hawatoi maziwa mengi lakini pia

ukienda mnadani hawanunuliwi kwa Bei nzuri , Ndipo nilielewa kuwa unachokitunza kinatunza pia , unachokitelekeza kinakutelekeza, unachokijari kitakujari pia , unachokipenda kitakupenda hii ni kanuni ya reprocity ndiyo maana hata maua yakitunzwa na kumwagiliwa vizuri hutoa hewa nzuri na mazingira mazuri ya binadamu kuishi lakini yakiachwa yanakauka na utapigwa na jua la kukutosha tu.

Ukitaka kula vya watu Lazima watu wale kutoka kwako pia , sio ule peke yako. Ukitaka kula peke yako tu, ujue kuna mahali hutaweza kufanikiwa kabisa. Hii ndiyo sheria kuu ya kurejeshewa unachokitoa (the law of reciprocity); unachokitunza na kukilisha, ndicho kitakachokuja kukutunza na kukulisha mbeleni.

Ukiwa bahili na usitoe pesa kwa watu wengine kwenye biashara, ujue biashara yako

haitatanuka. Mfano kitendo Cha kumwamini mtu mwingine na kumpa pesa akufanyie biashara Inaweza kuwa risky lakini, lazima ukubali wengine wafaidi na kupata mkate wao kupitia pesa zako pia, maana hakuna mtu anayekuja kwako asipate faida yoyote akabaki. Kwa hiyo, ni muhimu sana kufahamu kuwa unapofanya biashara haufanikiwi peke yako, bali mafanikio yako yanabeba na kufanikisha maisha ya wengi pia.

**Kanuni Ya Kugawana Utajiri**

Kuna siku tulikuwa tunapiga stori na tajiri mmoja. Yeye huwa anawapa pesa vijana wanaenda kununua mazao vijijini, halafu yeye anabaki mjini akisubiri mzigo. Sasa nikawa namuuliza, "Vipi kiongozi, unawaamini sana hao vijana? Maana vijana wengi siku hizi hawana uaminifu, wanaweza kukulagai na

kukuibia fedha zako." Akasema, "Ndugu yangu, maisha tunagawana kidogo kidogo tunachopata. Ukiwa mkazaji (bahili au mgumu) sana huwezi kutoboa. Sasa utafanya biashara gani duniani ambayo haina changamoto au watu wanaotafuta upande wao? Ni nani atakubali kukufanyia kazi halafu yeye asipate faida yoyote kabisa? Kwa hiyo lazima kuwe na balance of nature (urari wa asili); mwingine apate kipande hiki, na wewe chukua hiki. Mimi ninawapa pesa za kununua gunia 200 za mpunga, na kwa bei niliyowaambia wanunue, iwapo wakipunguziwa huko vijijini, hiyo inakuwa ni faida yao huko waliko. Lakini pia lazima niwalipe fedha ya nauli, chakula, pamoja na posho yao kwa sababu ya kazi hiyo. Ndio maana ya maisha kaka; tunasaidiana wote, kikubwa ni kufikia hatima zetu."

Nilijifunza kitu kikubwa sana pale, na mtazamo wangu kuhusu maisha ulianza kubadilika kabisa. Ndiyo maana nikasema, mafanikio yako si kwa ajili yako peke yako, bali kuna watu wanayasubiri lili na wao wainuke. Ndio maana ni muhimu sana kutokukata tamaa mapema; kuna watu wengi sana nyuma yako wanakutazama kama kioo chao. Sio kwamba hawawezi kufanikiwa peke yao, bali kwenye balance of nature, binadamu wote tunategemeana sana na kutegemezana kupitia sheria hii ya kurejeshewa ukarimu (the law of replocity).

## Unachokitunza Ndicho Kitakachokutunza

Hekima ya maisha inatufundisha kuwa kile unachokilinda, kukithamini, na kukistiri kwa uaminifu ndicho kinachojenga ukuta wa kukutunza wewe siku ya dhoruba. Ukilitunza

jina lako na uaminifu wako mbele ya watu leo, uaminifu huo utakuwa ngao yako kesho pindi maadui watakapokuandama. Ukizitunza na kuzilinda siri pamoja na madhaifu ya wale walio chini yako bila kuwadhalilisha, unajenga hazina ya heshima itakayokutunza pindi na wewe utakapofika hatua ya kuishiwa au kuanguka. Mtu anayeacha kulinda misingi yake ya utu na uaminifu kwa sababu ya tamaa ya haraka, anavunja paa la nyumba yake mwenyewe; kwani sheria ya reciprocity haidanganyi—kile unachokipa nafasi ya kuishi ndani ya moyo wako, ndicho kitakachokupa hifadhi siku ya shida

**Unachokilisha Ndicho Kitakachokulisha**

Mkulima anayeitunza ardhi kwa kuipatia mbolea na maji, ana uhakika wa kulishwa na ardhi hiyo hiyo wakati wa mavuno. Vivyo hivyo,

ukiwalisha vijana wanaokusaidia kwa kuwapa maslahi mazuri, kuwajali, na kuwapa nafasi ya kufurahi chini ya kivuli chako, unakuwa unalisha mizizi ya mti utakaokuzalishia matunda ya utajiri wa kudumu. Tajiri anayewafanya wafanyakazi wake wawe na njaa huku yeye akishiba peke yake, anapalilia sumu itakayokuja kuharibu ghala lake. Unapofungua mkono wako ili wengine wapate riziki kupitia wewe, unakuwa umeiwekea biashara yako bima isiyoonekana kwa macho; wale uliowalisha kwa upendo watakuwa tayari kupambana usiku na mchana kulinda kisima chako kisikauke, kwani wanajua kuwa kukauka kwako ni njaa kwao, ukiwawatunza wanao na kuwajari, kuwapa elimu nzuri , kuhakikisha maihitaji yao hayakosekani watoto hao watakutunza huko mbeleni ukiwa umezeeka huwezi tena kufanya

kazi, ukiwaacha na kuwatenga huko mbeleni wataimba wimbo wa nani kama mama.

**Unachokiheshimu Ndicho Kitakachokutukuza**

Kuna siri kubwa katika kuheshimu viwango na nafasi za watu wengine hata kama wako chini yako kiuchumi. Ukiiheshimu kazi ya mtu anayekubebea mizigo au anayekusafishia ofisi, unajenga mazingira yanayomfanya naye aiheshimu mamlaka yako kwa dhati na si kwa uoga. Sheria ya kurejeshewa heshima inasema kuwa huwezi kuvuna utukufu mahali ambapo ulipanda dharau. Watu waliofanikiwa na kudumu kileleni ni wale wanaojua kuwa dharau kwa mtu mdogo ni sawa na kutoboa mtumbwi unaosafiria. Hakikisha kila anayekanyaga kizingiti cha maisha yako anaondoka akiwa na utu wake ukiwa salama; heshima unayoitoa kwa

wengine leo ndiyo itakayojenga jukwaa la wewe kutukuzwa na vizazi vinavyokuja.

## Unachokisamehe Ndicho Kitakachokupa Amani

Mwisho wa siku, katika mchezo huu wa zaidi ya dakika tisini wa maisha, utakutana na wapigaji, wasio waaminifu, na watu watakaotumia mikono yako ya ukarimu kujinufaisha. Hata hivyo, ukiitunza hasira na kisasi moyoni mwako, utajaza sumu inayokuzuia kuona fursa mpya. Ukisamehe makosa madogo madogo ya kibinadamu na kukubali kuwa kupoteza kidogo ni sehemu ya kuifundisha asili, unajenga amani ya akili inayokupa nguvu ya kusonga mbele. Kusamehe hakuondoi uhalisia wa kosa, bali kunakutunza wewe usishikwe mateka na yaliyopita. Tunza amani yako ya ndani kwa kuachilia yasiyobadilika, kwani roho iliyo huru

ndiyo pekee yenye uwezo wa kuvuta utajiri mkubwa na kukamilisha mpangilio mzuri wa divine balance of nature.

## SURA YA KUMI: KUWA NA KIASI KWA KILA JAMBO NI HEKIMA (BALANCE OF EVERYTHING IS WISDOM)

Kula chakula ni kuzuri, lakini ukila sana utavimbewa na kuumwa tumbo. Kulala ni kuzuri, lakini ukilala sana utakuwa maskini. Kufanya kazi ni kuzuri, lakini ukifanya kazi sana utachoka na kuishiwa nguvu. Kuomba ni kuzuri, lakini kuombaomba ni kubaya. Kukesha ukiomba ni kuzuri, lakini usipolala kwa siku kadhaa utaugua.

Mtu mwenye hekima zaidi kuliko wote duniani (Suleimani katika Mithali 30:8) alisema: "Mungu usinipe utajiri wala umasikini; nisiwe tajiri sana nikakusahau Mungu wangu, na nisile chakula kingi sana nikashiba nikakufuru. Lakini pia nisiwe maskini sana nikatamani kuiba. Nipe chakula cha kunitosha nisiwe na uhaba, na nipe

utajiri ninaoweza kuumudu."(Ziada msisitizo zaidi)

Kumbuka kuwa Sulemani alikuwa mtu tajiri kupita wote duniani, lakini ilifika hatua akasema, "Ubatili, ubatili mtupu; mambo yote ni ubatili na kujilisha upepo." Kitu kikubwa sana alichogundua Sulemani ni kwamba, urari wa kila kitu ndio hekima (balance of everything is wisdom). Kitu chochote kikiwa kikubwa kupita kiasi ni kibaya. Haijalishi ni kitu gani kizuri, mradi kikiwa too much, kinaanza kuboa. Ndio maana ni muhimu sana kubalansi.

** Ukipenda sana, utachukuliwa mtu wa kawaida.*

** Usipojua kupenda, hutakuwa na mtu yeyote kwenye maisha yako.*

** Ukijali sana, unaonekana kama zezeta.*

** Usipojali kabisa, hutakaa na mwenzi kamwe kwenye maisha yako.*

** Ukijitoa sana, unaonekana unajipendekeza.*

** Usipojitoa kabisa, unakimbiwa chapuchapu.*

** Ukisaidia sana, utakuwa maskini.*

** Usiposaidia kabisa, hutasaidiwa pia.*

** Ukifikiria sana, utakufa na stress.*

** Usipofikiri kabisa, maisha yako hayataenda mbele.*

** Ukinenepa sana, utakufa na shinikizo la damu (pressure).*

** Ukikonda sana, watasema unaumwa.*

** Ukilala sana, utakufa maskini.*

** Usipolala kabisa, utaugua.*

Balance of everything is wisdom. Ukitaka kufurahia maisha yako ya kila siku kimwili na kiroho, jaribu kubalansi kila kitu. Usizidishe kiwango kwenye kila jambo (don't be much in everything). Usile sana, usiombe sana kupita kiasi cha kutelekeza majukumu, usitumie pesa sana, usiweke akiba sana hadi unajinyima, usisaidie watu kupita kiasi hadi unajiumiza, na usiwapuuze watu kupita kiasi. Balance of everything is wisdom.

Hekima kupita kiasi ni kuongeza huzuni. Nilishangaa sana Sulemani anaposema: "Usiwe na hekima kupita kiasi, kwani kujiangamiza mwenyewe." Yaani katika wingi wa hekima, kuna wingi wa huzuni pia. Hili nimeliona kabisa mimi mwenyewe; kuna muda ukikaa unajikuta huna raha tu, maana unaona makosa mengi sana yanayofanywa na jamii. Ndipo unaanza kuona

ujinga mwingi sana unaofanyika kwenye jamii, na mwisho wa siku unaishia kusema kama Sulemani: "Ubatili, ubatili mtupu." Ndiyo maana Sulemani akasema hata hekima iwe kwa kiasi pia, maana hutayafurahia maisha ukiwa na hekima kupita kiasi, na utaishi maisha ya huzuni muda mrefu sana.

**Furahia Kila Hatua Unayopiga Kwenye Maisha (Enjoy Your Life While Living)**

Kuna balaa kubwa nimeliona hapa duniani; yaani kuna mtu ambaye yuko busy sana kutafuta pesa ili aje aishi vizuri, lakini anasahau kuishi sasa hivi. Halafu akija kuzipata hizo pesa za kuishi, tayari muda wake wa kuondoka duniani unakuwa umefika. Hivyo, anaziacha hizo mali zote kwa watu wengine ambao hawajazitafuta. Huu ndio ubatili haswa.

Kuna balaa jingine nimeliona hapa duniani, nalo ni hili: Kuna matajiri wengi sana wako kijijini wanaishi maisha kama watu maskini, na kuna maskini wengi sana wako mjini wanaishi maisha kama watu matajiri. Hili nalo ni balaa kubwa. Yaani, hii inamaanisha kuna wale watu kule kijijini wanaishi maisha magumu sana, hata kama wana ng'ombe 200 lakini utakuta wanakula kwa tabu, wanalala pabaya, na makazi yao ni mabovu wala hayavutii kabisa. Ilihali wana uwezo wa kuishi vizuri sana jinsi wanavyotaka, lakini kwa ukosefu wa hekima, wanajikuta wanaishi maisha magumu kama maskini.

Lakini, kuna watu wengi sana mjini utakuta ana kipato kidogo sana—hata mshahara wake haufiki hata laki sita. Lakini amepanga chumba kimoja, akaweka sofa sebuleni, akanunua

kitanda kizuri, analala pazuri, na anakula vizuri pia, wakati huo kipato chake ni kidogo sana kiuhalisia. Lakini hajaacha kuishi vizuri na kujali afya yake.

Ndiyo maana Sulemani akasema katika Mhubiri 6:1-3 (Biblia Takatifu):

"***Kuna baa nililoliona mimi chini ya jua, nalo linawalemea wanadamu kwa uzito; mtu aliyepewa na Mungu mali, ukwasi, na heshima, hata asipungukiwe na kitu cho chote kwa nafsi yake, katika yote anayoyatamani walakini Mungu hamwezeshi kula katika hizo; bali mgeni hula. Hayo ndiyo ubatili hasa, nayo ni ugonjwa mbaya. Mtu akizaa watoto mia, akaishi miaka mingi, nazo siku za maisha yake ni nyingi, lakini nafsi yake haikushiba mema; tena ikiwa, zaidi ya hayo, amekosa maziko;***

***mimi nasema, Heri mimba iliyoharibika kuliko huyo."***

Nimekuja kugundua kuwa kwenye maisha, hakikisha unafurahia kila hatua unayopiga hata kwenye utafutaji wako. Usijinyime sana, wala usile bata sana; lakini furahia kila hatua MUNGU aliyokupa. Siku hazigandi na wala muda haukusubiri. Ukisema ujinyime—yaani uwe bahili hutoi kwa watu, na wala wewe mwenyewe hujijali—ujue kabisa kuna siku utaondoka na utaacha kila kitu.

Sulemani akasema hakuna kitu kizuri kupita kula na kunywa na kuuburudisha moyo wako kwa mema(mhubiri 2:24). Yaani, hakikisha unafurahia kila hatua unayopiga, lakini pia saidia watu wengine kama ukiwa na uwezo wa kumsaidia. Usiwe bahili kupita kiasi kwani ni kujiangamiza mwenyewe.

Kama una uwezo wa kumlipia mwanao ada, na mtoto wa jirani yako au yatima akapata msaada na chenji ikabaki, basi fanya hivyo. Hakika kuna raha yake katika kusaidia wengine. Sulemani anasema hakuna furaha kama hiyo—yaani kusaidia mayatima na wajane—maana unakuwa umemsaidia MUNGU kazi. Maana Yeye anaposema "nitakuinulia watu na kabila za watu," basi wewe unakuwa huyo mtu unayetimiza neno la MUNGU kwenye maisha ya watu WINGINE. Na maandiko yakasema, mtu ambaye anasaidia watu wengine, anamkopesha MUNGU

*Mithali 19:17 Amhurumiaye maskini humkopesha Bwana; Naye atamlipa kwa tendo lake jema*.

**Falsafa ya "Kipimo cha katikati (The Divine Geometry of Balance)**

Uzuri wa mduara wa maisha hautokani na mistari kunyooka kwenda juu sana au chini sana, bali unatokana na uwezo wa kukaa kwenye kitovu cha katikati. Hekima kubwa haipo kwenye kuwa na kila kitu, bali ipo kwenye kujua kiwango kinachokutosha bila kuharibu amani yako ya roho. Ndege anayeruka juu sana anajisogeza karibu na hatari ya radi, na anayeruka chini sana anajisogeza kwenye mitego ya wawindaji; maisha ya ushindi yanapatikana pale unapojua kuruka umbali wa katikati unaokupa uhuru na usalama kwa wakati mmoja. Unapojua kubalansi, unajifunza kuishi kama msafiri mwenye akili anayefurahia mandhari ya safari bila kulemewa na uzito wa mizigo yake.

**Hatari ya "Kesho Inayouwa Leo" (The Illusion of Tomorrow)**

Siri kubwa ya kupoteza furaha duniani huanza pale mwanadamu anapoweka rehani "leo yake ya sasa" kwa ajili ya "kesho isiyojulikana". Tunajenga maghala makubwa ya kesho huku miili na nafsi zetu zikiteseka na njaa ya upendo na burudani leo. Kupanga kwa ajili ya kesho ni hekima, lakini kuikataa leo kwa hofu ya kesho ni ugonjwa mbaya wa kisaikolojia unaowatafuna matajiri wengi waliobahilika. Furahia kikombe cha kahawa ulichonacho sasa, cheka na watoto wako leo, na lala kwa amani usiku huu; kwani maisha yanaundwa na mfululizo wa nyakati za "sasa" na hakuna mtu aliyewahi kuishi ndani ya kesho.

**Utajiri wa Roho Dhidi ya Ufukara wa Mali (The Poverty of Having Money)**

Kuna tofauti kubwa sana kati ya mtu mwenye pesa na mtu aliye tajiri; kuwa na pesa kunajaza akaunti ya benki, lakini kuwa tajiri kunajaza nafsi na utu wa mtu. Mtu anayemiliki mamilioni lakini akashindwa kutoa nusu yake kuokoa maisha ya yatima, au akashindwa kulala vizuri kwa hofu ya kuibiwa, huyo ni fukara aliyevikwa joho la dhahabu. Hekima ya asili inatufundisha kuwa, thamani ya mali zako haipimwi kwa kile ulichokifungia kwenye sefu yako, bali inapimwa kwa kiwango cha tabasamu ulizoweza kuzitengeneza kwenye nyuso za watu waliokata tamaa kupitia mali hizo.

Ukitembea kwenye makaburi ya watu mashuhuri na matajiri waliowahi kutikisa dunia, utagundua kuwa sote tunashuka ardhini tukiwa na ukubwa wa sanduku lile lile moja la udongo. Hakuna

gari la kifahari linalomfuata tajiri kaburini, na hakuna nyumba ya ghorofa inayomkinga na baridi ya ardhini. Ushahidi pekee unaobaki duniani baada ya wewe kuondoka ni alama ya wema uliouacha kwenye mioyo ya wanadamu na msaada ulioutoa kwa wale wasiojiweza. Kuwa mkarimu kwa maisha yako, ishi kwa furaha, na kuwa mkono wa MUNGU kwa wajane na mayatima; kwani huko ndiko kujiwekea akiba ya milele mahali ambapo mchwa na kutu hawawezi kuharibu.

Kama ayubu alivyo kuwa yeye alikua miguu kwa viwete, na mdomo kwa bubu, baba wa yatima na mume kwa wajane maana alihakikisha hawatoi machozi mbele yake hao watu wanyonge.

*Ayubu 29:12-16 (Biblia sTakatifu) Kwa sababu nalimwokoa maskini aliyenililia; Yatima naye,*

*na yule asiyekuwa na mtu wa kumsaidia. Baraka yake yeye aliyekuwa karibu na kupotea ilinijia; Nikaufanya moyo wa mjane kuimba kwa furaha.Nalijivika haki, ikanifunika, Adili yangu ilikuwa kama joho na kilemba. Nalikuwa macho kwa kipofu, Nalikuwa miguu kwa aliyechechemea.Nalikuwa baba kwa mhitaji, Na daawa ya mtu nisiyemjua naliichunguza.*

## SURA YA KUMI NA MOJA: MWENYE KISU KIKALI NDIYE MLA NYAMA (SURVIVAL FOR THE FITTEST)

Siku moja nilienda kwa muuza maziwa kwenda kuchukua maziwa mgando nikamkuta yule muuza maziwa ndoo nzima ya maziwa imeharibika yaani yamechacha na hivyo hawezi kuyauza tena kwa mtu yoyote. Nikamuuliza, "Kwa hiyo kama yakiharibika haya maziwa, huwa mnafanya nini?" Akasema, "Huwa tunayarudisha kwa wenye nayo kijijini halafu wanatuma mengine." Nikauliza, "Lakini si inakuwa ni hasara kwenu?" Akasema, "Ndio maana kama yakimaliza siku nyingi sana hayajanunuliwa yanaharibika na huwezi kumuuzia mtu maziwa yaliyoharibika tayari."

Nilipoondoka mahali pale, Roho wa hekima akaanza kuzungumza ndani yangu: Unaona jinsi watu wengine wanavyopata taabu ku-survive

hapa duniani? Huyu mtu unayemwona ana mtoto yuko shule, ana familia, inabidi alipe ada ya shule, familia ile ishibe na mambo mengine ya kijamii; unadhani anaishi vipi kwa kutegemea hayo maziwa tu?

Lakini kwa hekima ya MUNGU, hawa watu wote MUNGU huhakikisha wanakula na kukidhi pia mahitaji yao. Japokuwa wewe umeona taabu anayoipata huyo mtu, lakini MUNGU anajua atakavyomlisha na kuhakikisha haki zake zote anapata kama mtoto wa MUNGU.

Hapo ndipo nikaelewa vizuri maana halisi ya divine balance of nature. Hekima ya MUNGU haichunguziki. Ndipo nilielewa kwa nini YESU alisema kunguru hawapandi wala hawavuni lakini MUNGU huwalisha. Ndipo nilielewa kuwa kuna vichaa mtaani hawana shamba wala hawavuni lakini MUNGU huwalisha pia na

wana-survive hapa duniani. Kuna watu wengi sana wako mjini wanaishi maisha ya kusaidiwa na MUNGU mwenyewe.

Fikiri mtu anauza nyanya sokoni, nyanya zinakosa wateja zinaharibika zote halafu kesho tena anaagiza nyanya zingine; swali: huyu mtu anaishi vipi? Au mtu anayeuza samaki, baada ya siku kadhaa samaki huchina na hakuna mtu wa kuwanunua tena; swali: anaishi jaje huyu mtu? Ndipo kauli ya MUNGU inakuwa halisi anasema, "Njia zangu hazichunguziki wala mawazo yangu siyo kama mawazo yenu."

Nilichokuja kugundua kwenye maisha yetu ya kila siku, hata kuwe na njaa kiasi gani, hata kama kuwe na ugumu wa maisha kiasi gani, MUNGU atahakikisha unapata chakula. Ndiyo maana kuna watu wengi mtaani hawana pesa ya shamba, hawana pesa ya kulipia kodi, hawana

pesa ya kuanzia biashara lakini hawezi kukosa 1,000 au 2,000 ya kula; ndio wanaitwa wasaka tonge. Hili kila mtu ana ushahidi katika maisha yake mwenyewe. Yaani kuna kipindi hukuwa na chochote kabisa lakini ulikula, hata kama ni mkate na chai, au andazi moja ukalala lakini ulikula. Ni ngumu sana MUNGU kuruhusu mtoto wake alale njaa ndio maana akasema hata ndege wa angani hawapandi wala hawavuni lakini MUNGU huwalisha, sembuse wewe mtoto wake. This is the meaning of balance of nature.

**Mwenye kisu kikali ndiye mla nyama (Survival of the fittest)**

Kwenye maisha yetu ya kila siku lazima kuwe na nyasi, swala, na simba. Ninaposema nyasi ninamaanisha watu wa hali ya chini kabisa ambao hukanyagwa na kila mtu yaani hawana

misuli ya kiuchumi kabisa; watu wanaishi chini ya dola moja. Siyo MUNGU aliyewaweka lahasha, bali mazingira yamewaweka kwenye hali hiyo. Na MUNGU mwenyewe hapendi kabisa watu wawe chini kimaisha lakini nature imewapeleka huko, mfano mayatima, watoto wa mtaani, watu wasio na chanzo cha mapato chenye uhakika kabisa.

Ninaposema swala namaanisha watu wa hali ya kati ya maisha ambao kidogo wanafanya kazi nzuri na kulipwa mshahara mzuri, wanaweza kujenga nyumba nzuri na kusomesha watoto wao yaani siyo wanyonge sana kwenye maisha, wana uchumi wa kati. Lakini bado na wao pia ni vitoweo vya simba; ni vitoweo vya watu wengine walio juu yao na hawawezi kuishi bila msaada wa watu walioko juu maana wanafanyia kazi hao simba (watu wenye misuli ya

KIUCHUMI). Kwa hiyo, japokuwa wanaonekana kuwa na maisha mazuri lakini bado na wao ni vitoweo vya watu wengine.

Ninaposema simba, hawa ni watu wenye misuli ya KIUCHUMI. Wana makampuni makubwa, wanatoa ajira kwa wengine, wao hawaliwi na watu wengine (yaani hakuna mtu anayewanyonya maana wanajitegemea kwa kila kitu), hawategemei msaada wa watu wengine ila wanategemei nguvu kazi ya watu wengine ili maisha yao yaweze kusonga mbele.

Sasa kama ambavyo kwenye msitu hakuna siku itatokea kusiwe na nyasi, swala, na simba, ndivyo ambavyo kwenye maisha yetu ya kila siku hakuna siku itatokea kusiwe na watu wa chini kabisa kwenye maisha (nyasi), watu wa kati (swala), na watu wa hali ya juu kiuchumi (simba). Kwa sababu, according to the balance

of nature, kama nyasi zote zikikauka basi swala wote watakufa na simba nao watakufa maana hawana chakula. Kuna mtu anaweza kusema, "Kwani lazima ale swala tu, simba anakula vingi?" Kumbuka ujumbe wangu mkuu wa watu wa hali ya chini, hali ya kati, na hali ya juu kiuchumi na kimaisha pia. Kwa hiyo, iwe ni kundi jingine tofauti na swala, lakini naposema simba namaanisha mnyama anakula wanyama wenzie na mtawala wa mwituni. Kwa hiyo wanyama wote wanaoliwa na simba wanasimama kwenye kundi la swala. Hiyo ndio inaleta maana ya watu wote walioajiriwa, wanaofanya kazi za watu wengine ili walipwe mshahara au kipato chao; wanasimama kwenye kundi la swala yaani kuna watu juu yao wanaowanyonya, wanategemea nguvu kazi yao ili kufanikisha biashara zao, makampuni yao n.k.

Na wale watu wenye uhuru wa KIUCHUMI ndiyo wanasimama kama simba. Hawawezi kuishi bila msaada wa watu wengine, hasa wale wenye hali ya kati kiuchumi. Wakati huo watu wanaofanya kazi ya day worker, kutembeza nguo, vitumbua, na wengine mayatima kabisa hawana wazazi wala dira yoyote ile ya kimaisha wanasimama kwenye kundi la nyasi—watu wa hali ya chini kabisa kwenye maisha, wengi wanawaita watu wanaoishi chini ya dola moja.

Swali linakuja: nani awe nyasi, nani awe swala, nani awe simba? Je, ni mapenzi ya MUNGU watu wengine wawe chini kabisa kwenye maisha? Lahasha, MUNGU hakumuumba mwanadamu aishi kwa mateso bali kila mtu aliumbwa kutawala na kuwa na vitu vyote. Lakini Adamu na Hawa walipotenda DHAMBI YA UJANA kule Edeni mambo yalibadilika;

hatutakuwa sawa tena kwenye maisha maana aliambiwa, "Kwa jasho lako utakula." Kwa lugha rahisi, unatakiwa ufanye juhudi kubwa ili ufanikiwe kwenye maisha. Utasoma kitabu cha Madhara ya Dhambi ya Ujana uelewe madhara ya dhambi pale Edeni. Kuna vitu saba vilivyozaliwa baada tu ya kutenda DHAMBI YA UJANA kule Edeni.

Kwa hiyo MUNGU anaposema utakula kwa jasho, tafsiri yake utaratibu wa kuishi umebadilika. Itakubidi ufanye juhudi kubwa ili ufanikiwe, ndiyo maana mpaka sasa watu wenye hekima, bidii, na maarifa mengi ndiyo hushika nafasi za juu yaani simba, na wale wenye mikono milegevu hubaki kuwa watu wa hali ya chini kabisa kwenye maisha. Ndiyo maana Sulemani akasema:

*Mithali 22:29 (Biblia Takatifu) Je! Wamwona mtu mwenye bidii katika kazi zake? Huyo atasimama mbele ya wafalme; Hatasimama mbele ya watu wasio na cheo*.

Kwa lugha nyingine, Sulemani alisema MUNGU hana tabia ya kumwambia mtu awe simba au awe swala, bali wao wenyewe kulingana na maamuzi waliyofanya wao au wazazi wao, na juhudi zao binafsi huwa-classify kuwa kwenye kundi jingine tofauti kimaisha. Ndiyo maana akasema mwenye bidii huyo atatoka kwenye kundi la watu wa hali ya chini kabisa kwenye maisha bali wale wa juu (simba = wafalme).

Ndiyo maana Sulemani akasema tena:

***Mithali 22:2 (Biblia Takatifu) Tajiri na maskini hukutana pamoja; Bwana ndiye aliyewaumba wote wawili***.

Hakusema BWANA ndiye aliyewaumba hivyo, bali ndiye aliyewaumba wote. Yaani MUNGU aliwaumba wakiwa na nafasi sawa kila mtu ya kufanikiwa kuwa tajiri, lakini baada ya muda wakaja kukutana mwingine kashakuwa simba mwingine akiwa swala. Lakini wote wanategemeana kuishi. Kwa hiyo lazima tuelewe kwamba MUNGU hakumuumba mtu tajiri au maskini, bali aliumba watu lakini hao watu wanajigawanya wao wenyewe kulingana na maarifa uliyonayo na juhudi zao binafsi. Ndio maana kuna sehemu Sulemani akasema:

***Mithali 10:4 Atendaye mambo kwa mkono mlegevu huwa maskini; Bali mkono wake aliye na bidii hutajirisha***.

Na kwa sababu hiyo, tajiri (simba) automatically humtawala maskini (swala) kwa sababu ya nature ya maisha:

*Mithali 22:7 (Biblia Takatifu) Tajiri humtawala maskini, Naye akopaye ni mtumwa wake akopeshaye*.

Yaani mtu ambaye yuko vizuri sana KIUCHUMI, yupo kwenye level ya juu sana ni simba, huyo lazima atamtawala aliye chini kabisa kwenye maisha (swala) na kumtumikisha. Siyo mapenzi ya MUNGU lakini huyu maskini ili aishi atalazimika amtumikie tajiri alipwe mshahara alishe familia yake, anunue na kiwanja n.k. Lakini hata huyo mtu maskini bado ana nafasi yake ya kuwa tajiri ndiyo maana Sulemani akasema:

***Mithali 22:22-23 (Biblia Takatifu) Usimnyang'anye maskini, kwa kuwa ni maskini; Wala usimdhulumu mtu mnyonge langoni; Kwa sababu Bwana atawatetea; Naye atawateka uhai wao waliowateka***.

Ukiwa hali ya juu KIUCHUMI usianze kunyanyasa walio chini yako. Lazima uelewe kuwa hata walioko chini kabisa kwenye maisha ni watu wa MUNGU pia, siku yoyote ile watakuwa juu. MUNGU anatambua uwepo wako na uwepo wao pia; yeye mwenyewe ndiye aliyetuumba sote, tu kazi ya mikono yake na tuna-balance nature.

Hata YESU alipokuja DUNIANI alisema kwenye maisha wanaokuwa juu (level ya ufalme) ni watu wenye misuli, watu wenye nguvu, na kila mtu ana uhuru wa kufanikiwa kuwa mtu mkuu lakini inahitajika nguvu ya ziada, sio kukaa kizembe.

***Mathayo 11:12 (Biblia Takatifu) Tangu siku za Yohana Mbatizaji hata sasa ufalme wa mbinguni hupatikana kwa nguvu, nao wenye nguvu wauteka.***

Haupati mafanikio kizembe, kivivuvivu, bali kuna juhudi kubwa sana kwenye ufalme. Tunaposema ufalme ni hali ya juu kabisa KIUCHUMI, kisiasa, kimaisha kiujumla. Ndio maana hata darasani ili upate ufaulu wa juu yaani division one lazima kuna kukesha, ukisoma kitabu, kufanya kitu cha ziada tofauti na ratiba ya darasani. Watu wote wanaofanikiwa kwenye maisha ni wale wanaofanya kitu cha ziada tofauti na ratiba za majukumu ya kawaida. Ndiyo maana hata MUNGU mwenyewe akasema ufalme wa MUNGU hutekwa na wenye nguvu (nguvu ya maarifa, nguvu za rohoni, nguvu za mwilini).

**HITIMISHO**

Kwa ujumla kitabu hiki divine balance of nature kinatukumbusha kuwa ulimwengu haukutokea kwa bahati mbaya ,kila kiumbe ,kuanzia mdudu mdogo hadi mabadiriko ya majira ,kimeumbwa kwa hekima kubwa na kina umuhimu wake katika kuitengeneza dunia . usawa huu wa kimungu ni kioo kinachoonyesha umuhimu wa kuishi kwa maelewano, Amani, na kuheshimiana tunapoharibu asili, tunaharibu maisha yetu wenyewe, wajibu wetu mkuu kama wanadamu ni kuwa walinzi wema wa mfumo huu mzuri, tukiwa na urithi salama kwa vizazi vijavyo na kuenzi hekima ya MUNGU iliyofichwa katika kona ya sayari yetu.

Kitabu hiki kimejikita katika kuileza hekima ya MUNGU katika uumbaji na umuhimu wa

kuelewa mapungufu yetu na mipaka yetu tuliyonayo ili kuishi kwa Amani na watu wote ikiwa tunatambua ya kuwa siku za kuishi kwetu hapa duniani ni chache sana, yaani mwanadamu anayeweza kuishi siku nyingi sana duniani ni siku 36500 ni sawa na  miezi 3033 tu na sawa na wiki 5200 tu ,